SUPA JACKPOT
TZS. 1,074,741,067
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Wanaokeketwa** wadai kunaswa na zawadi siku ya kutoka

UKURASA 3




ELIMU
NA PANKRAS LUOGA

IONE HATARI HII

**Mabegi makubwa, mazito kwa mwanafunzi ni kumwandaa...**

• Kusagika pingili mgongoni, ubovu wa mabega, shingo, kiuno na miguu

NI mwanzo wa mwaka wa masomo, shule zimefunguliwa mwezi mmoja sasa. Mambo mengi yanayowasumbua wanafunzi wanaokwenda shuleni kutembea umbali mrefu kuifikia shule na kurudi nyumbani, njaa shuleni hakuna chakula hata maji ya kunywa.

Wanaoishi mijini tatizo la usafiri kwenye mabasi ya daladala na mwendokasi ni changamoto. Lakini pamoja na hayo upo mzigo mgongoni unaowasumbua wanafunzi wa msingi na sekondari ni mabegi makubwa na mazito wanayokukuruka nayo kila siku waendapo shuleni.

UKURASA 11

# Nipashe

Jumanne Februari 7, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581214
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

The Guardian digital
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US



# Tundu Lissu ataja aliko dereva wake

• **Asema** ameshalipwa nusu ya mafao ya ubunge, afunguka kinachoendelea ndani ya CHADEMA... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

**SAMIA ARIDHIA ENEO MAGEREZA KUMEGWA**

RAIS Samia Suluhu Hassan amemaliza mgogoro wa ardhi yenye ukubwa wa...

UKURASA WA 8

**WIZARA YAANIKA MAFICHO 8 YA MAUAJI**

WIZARA ya Mambo ya Ndani ya Nchi imesema matukio ya mauaji na ukatili...

## Wakazi Magomeni Kota wagomea kununua nyumba kwa mil. 56/-

UKURASA 3




Baadhi ya waombolezaji wakitoa heshima za mwisho kwenye majeneza yaliyobeba miili ya marehemu waliopata ajali ya gari eneo la Korogwe mkoani Tanga katika viwanja vya Hospitali ya Huruma wilayani Rombo mkoani Kilimanjaro kabla ya mazishi jana. **PICHA: MARY MOSHA**

# Ilivyozikwa miili ndugu 12 wa ajali

UK.5

**MICHEZO** SAKHO, BALEKE FITI KUIVAA HOROYA CAF UK.24
**KATUNI** UK.6

# Lissu ataja aliko dereva wake

**Na Elizabeth Zaya**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Bara, Tundu Lissu, amesema dereva wake anafanya kazi na kutunzwa na Serikali ya Ubelgiji.

Lissu alitoa kauli hiyo katika mahojiano maalum na kituo cha runinga cha ITV kupitia kipindi chake cha Dakika 45 kilichorushwa usiku wa kuamkia leo.

Amesema kama Jeshi la Polisi linamtaka, ni lazima liwasiliane na Shirikisho la Polisi la Kimataifa (Interpol) au kuandika barua kwa Serikali ya Ubelgiji ya kumhitaji kuja kusaidia kutoa ushahidi.

"Dereva wangu amekwenda Ubelgiji kwa sababu alipatiwa VISA ya kwenda huko na serikali hiyo, hakuwa hata na pasi ya kusafiria, lakini kwa sababu ya hali ilivyokuwa wakati ule, kwamba mimi nimeshambuliwa na waliofanya hivyo hawajatafutwa, maisha yake yako hatarini, kulikuwa na mambo mengi.

"Mimi nilipewa VISA ya matibabu, dereva wangu alipewa ya kibinadamu ili kuhakikisha kwamba anakwenda kukaa mahali salama. Mimi sijawahi kutunzwa na Serikali ya Ubelgiji, yeye anatunzwa na serikali hiyo, angalau mpaka amesoma lugha, ufundi, ameanza kazi sasa anaweza akajitegemea, lakini bila serikali hiyo asingeenda," Lissu alifafanua.



**ALIPWA MISHAHARA**

Lissu pia alisema anamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kutokana na serikali yake kumlipa kiinua mgongo chake cha ubunge cha miezi 24 kati ya 44 aliyotakiwa kulipwa na sasa anasubiri kulipwa gharama za matibabu.

"Mimi nilikuwa mbunge, nilifanya kazi hiyo miezi 44, takribani miaka minne. Nilipaswa nilipwe kiinua mgongo cha hiyo miezi, lakini hadi mwaka jana sijalipwa fedha yoyote ya kiinua mgongo," alisema.

"Rais alipokuja (Ubelgiji) akasema atashughulikia kiinua mgongo changu, wamenilipa cha miezi 24, siyo 44 na hicho walicholipa sijaona hata senti kwa kweli kwa sababu nilikuwa na madeni. Nimerudi ili waniambie fedha zangu za miezi 20 ziko wapi.

"Sheria ya Tanzania inasema mbunge akiugua nje ya nchi, anagharamiwa na Bunge na gharama zote zimewekwa kwenye nyaraka mbalimbali za serikali na za Bunge.

"Nilimwambia Rais kwamba 'wewe peke yako ndiye ulikuja Nairobi kuniangalia hospitalini, ulinionaje? Unajisikiaje kwamba nimehangaika hivi sijatibiwa na serikali kwa fedha ya umma kama inavyosema kisheria.

"Rais akaniambia 'andika barua uniambie ni kiasi gani ambacho umetumia, tutakulipa fedha zako'. Nimemwandikia, barua imekwenda na nimeambatanisha kila kitu, bado ninasubiri atekeleze ahadi yake," Lissu alisema.

**DEMOKRASIA**

Lissu alidai kulikuwa na jitihada za kuua demokrasia nchini, lakini Rais Samia amerejesha na 'sasa watu wanaongea'.

"Kulikuwa na jitihada kubwa za kuua demokrasia, hizo jitihada zimeshindikana. Haya ambayo anayafanya Rais Samia sasa hivi ni uthibitisho kwamba hizo jitihada za kuua demokrasia nchini zimeshindikana.

"Lakini ukiangalia kwa miaka 30, hali ya kisiasa imebadilika. Tanzania sasa ni nchi ya vyama vingi. Pamoja na jitihada zote za kukanusha hili, lakini demokrasia yetu imekua," Lissu alifafanua.

**URAIS 2025**

Lissu pia alionyesha nia ya kugombea tena nafasi ya urais katika uchaguzi mkuu ujao, lakini akaweka angalizo kuwa hilo atalifanya ikiwa Katiba Mpya itapatikana.

"Tunataka Katiba Mpya kwanza itakayohakikisha kwamba tuna Tume Huru ya Uchaguzi, tuna sheria mpya ya uchaguzi, tuna majimbo mapya ya uchaguzi. Haya yote yakikamilika, tuzungumze 2025. Yasipokamilika maana yake hali ya nchi hii itakuwa mbaya sana," alidai.

Alipoulizwa kama ana ndoto ya kugombea nafasi hiyo ya urais, Lissu alisema: "Ndoto ipo, ndoto ni ndoto tu. Lazima tuhakikishe kuna mazingira yatakayohakikisha hizo ndoto zinakuwa za kweli, bila Tume huru ya uchaguzi, tutakuwa watu wa ajabu sana kwenda kwenye uchaguzi".

**KATIBA MPYA**

Lissu pia alisema hoja kuu ya chama hicho bado itabaki kuwa ni Katiba Mpya mpaka itakapopatikana.

"Tukimpatia Rais muda hatutapata Katiba Mpya. Mara ya kwanza kwa nchi yetu kusema Katiba Mpya inahitajika ilikuwa ni mwaka 1991, miaka 32 iliyopita ambapo tume ya Rais ya mfumo wa chama kimoja au mfumo wa vyama vingi vya siasa iliyoongozwa na Jaji Mkuu Francis Nyalali ilipendekeza kwamba kama sehemu ya kuirudisha nchi katika mfumo wa vyama vingi, ni lazima kuwe na Katiba Mpya ya kidemokrasia.

"Na Tume ya Nyalali ilisema hivyo kwa sababu Katiba ya sasa kwa misingi na maudhui yake ni ya chama kimoja. Tusubiri mpaka lini? Mpaka wote waliokuwapo mwaka 1991 waondoke duniani?" Lissu alihoji.

Lissu alisema cha kwanza ambacho wanataka kianze katika mchakato huo wa Katiba Mpya ni kutungwa kwa sheria ya kurudisha mchakato.

Mtaalamu huyo wa sheria alidai kuwa sheria mbili zilizotungwa katika uongozi wa awamu ya nne zimekwisha muda wake.

"Hiyo sheria mpya lazima iseme tunaanzia wapi kwa sababu kuna kazi kubwa ilishafanyika tayari. Tuna rasimu ya (Jaji Joseph) Warioba na Katiba inayopendekezwa lakini mapendekezo yaliyomo kwenye zote hizo mbili ni tofauti," Lissu alisema.

**RASIMU YA WARIOBA**

Lissu alisema mapendekezo ya rasimu ya Jaji Warioba ndio yanatakiwa kuchukuliwa japo yanaweza kufanyiwa maboresho madogo kuliko Katiba inayopendekezwa.

"Katiba inayopendekezwa tukianze nayo maana yake ni Katiba ya sasa imepakwa rangi hivi na kuwekewa mwaka tofauti. Maana yake tutakuwa na Katiba Mpya kwa jina tu.

"Mapendekezo ya Warioba yana upungufu kidogo kama ilivyo kazi yoyote ya mikono ya binadamu, lakini yanaweza yakaboreshwa kwa sababu misingi yake ni tofauti na Katiba ya sasa.

"Kwa hiyo, sisi CHADEMA tunasema tuanze na alikoishia Warioba na tume yake, twende mbele. Kuna mambo mengi ambayo yametokea tangu mwaka 2013 rasimu ilipotolewa ambayo tukiangalia tunaweza kuboresha zaidi.

"Wapo watu ambao wanasema tuangalie na Katiba inayopendekezwa, hiyo inafanyiwa kazi kwa kushirikiana CHADEMA na CCM hivi tunavyozungumza, kuangalia tunafanya utaratibu gani wa kuhakikisha tunakuwa na waraka mmoja utakaokubaliwa na nchi nzima, kuangalia namna ya kurejesha mchakato relini," alisema.

**NDANI YA CHADEMA**

Alipoulizwa kuhusu kinachodaiwa kuwapo mpasuko ndani ya CHADEMA, Lissu alisema hakuna mpasuko, akidai kuwa hayo ni mambo yanayotengenezwa na baadhi ya watu.

"Kwenye Katiba yetu, hakuna mahali ambapo inasema mgombea wa nafasi ya uenyekiti anakuwa mgombea pekee halafu ndiye lazima awe Rais wa nchi, hakuna. Mwenyekiti anachaguliwa, anapingwa kama ilivyo kwa Makamu Mwenyekiti na viongozi wengine wote.

"Ni kweli hatuna ukomo wa madaraka katika nafasi za kuchaguliwa, miaka ya nyuma tulikuwa na ukomo wa madaraka, lakini kuna kipindi ilikuwa ni shida kupata viongozi wa kujaza nafasi mbalimbali. Lakini pia tuligundua kwamba ni vigumu watu kupata uzoefu katika nafasi hizo kwa kuweka ukomo, tukaondoa," Lissu alikumbusha.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
06.02.2023

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya **Alhamisi tarehe 09-02-2023** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam Port kuelekea Kilombero kupitia Mikumi,** gari hizo zina namba za usajili:
**T 203 DYJ / T 321 DDH / T 204 DYJ / T 310 DDH**
2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:
**Urefu - mita 23.00**
**Upana - mita 5.10**
**Kimo - mita 4.80**
3. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam, hadi Kilombero kupitia Mikumi,** gari itasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

217267202



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
06.02.2023

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya **Alhamisi tarehe 09-02-2023** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam Port kuelekea Rufiji,** gari hizo zina namba za usajili: **T 645 DFA / T 393 DVS / T 402 DFE / T 394 DVS T 578 BDZ / T 416 AYQ**
2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:
**Urefu - mita 23.00**
**Upana - mita 5.20**
**Kimo - mita 5.00**
3. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam, Pwani hadi Rufiji** kupitia Kibiti, gari zitasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

217267202

HABARI KITAIFA

# Wakazi Magomeni Kota wagomea kununua nyumba kwa Mil. 56/-

**Na Waandishi Wetu**

KAYA 644 za Magomeni Kota zimegoma kutia saini mkataba wa kuanza kununua nyumba hizo kuanzia Februari 8, mwaka huu kwa kile zinachodai sio rafiki kutokana na hali zao kiuchumi.

Wakazi hao pia wamemwomba Rais Samia Suluhu Hassan asikie kilio chao, wakidai bei ya serikali ya kati ya Sh. milioni 48 na Sh. milioni 56 haiendani na hali ya uchumi wao na maisha waliyonayo sasa.



Mwenyekiti wa wakazi wa Magomeni Kota, Geogre Abel, akizungumza na wakazi wa nyumba hizo kusikiliza malalamiko yao ya kupinga bei ya kununua nyumba hizo ambayo ni Sh. milioni 56 juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

Mwanasheria wa wakazi hao, Twaha Taslima, akisoma barua iliyoandikwa na Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Majengo Tanzania (TBA), Daud Kandoro kwenda kwa wakazi hao juzi kwenye eneo la mradi huo mkoani Dar es Salaam, alisema mkataba huo umeeleza masuala kadhaa. Alisema barua hiyo inaeleza kwamba bei iliyopendekezwa na serikali awali ilikuwa ni Sh. milioni 12 hadi 17, ikitolewa Juni mwaka jana, haikukidhi thamani ya eneo, haikujumuisha faida wala huduma za maeneo yanayozunguka makazi hayo ambayo ni jumuishi.

"Njia mojawapo ya kuchukua ni kuiomba serikali au kwenda mahakamani. Bei ya chumba na sebule kwa Sh. milioni 48 na vyumba viwili na sebule Sh. milioni 56.8 inaweza isiwe rafiki na mnunuzu asimudu," alidai Taslima.

Mwenyekiti wa Wakazi wa Magomeni Kota, George Abel, alidai bei zilizokokotolewa sio rafiki kwa wakazi hao licha ya serikali kuwaongeza mkataba wa kulipa na kuishi kutoka miaka 10 hadi 15.

Alisema kwa bei hiyo inatakiwa kila mkazi alipie Sh. 300,000 kwa mwezi, hivyo kwa mwaka ni Sh. 3,600,000 (milioni 3.6), akidai kiasi hicho ni kikubwa, ikizingatiwa baadhi ya wakazi tayari ni wazee na wastaafu.

"Tumepokea barua hii ikiwa zimebaki siku mbili tu - kwamba tusaini mkataba wa ununuzi, tukutane tujadiliane kabla ya Februari 8 mwaka huu. Hizi bei sio rafiki, haziendani na hali za wakazi walio wengi," alidai Abel.

Mmoja wa wakazi wa nyumba hizo, Salama Goronga (65) alisema barua hiyo iliyosomwa kwao ikionyesha bei hiyo, imewahuzunisha kwa kuwa haiendani na hali zao kimaisha.

"Mimi nina wajukuu na iliposomwa barua, machozi tu yameanza kunitoka, hiyo fedha nitatoa wapi? Nitaondoka hapa niende wapi?" Salama alihoji.

Mkazi mwingine, Mwajuma Hamisi (82) alisema ana watoto wawili walioolewa na ndio wanaomtunza kwa kumnunulia chakula na mahitaji mengine, hivyo itawawia ugumu kumtafutia malipo kwa ajili ya ununuzi wa nyumba hizo, hivyo ni wazi ataondolewa kwenye makazi hayo kutokana na kushindwa kulipa.

"TBA wanaotaka hizo nyumba, leo bei hii, kesho hii, tutalipaje? Mimi mzee, wanitoe hapa ni aibu kwangu, mamilioni hayo nitayatoa wapi?" alihoji Mwajuma.

# Wanaokeketwa wadai kunaswa na zawadi

**Na Kulwa Mzee**

WANAFUNZI wa shule za sekondari na msingi wameibua hoja mpya kuhusu ukeketaji, wakidai zawadi wanazopewa na wazazi wakati wa sherehe za ukeketaji zikiwamo fedha ndizo zinazowashawishi baadhi ya mabinti kukubali kukeketwa.

Hayo yalibainika jana wakati wa mdahalo wa kupinga ukeketaji uliohusisha shule mbili za sekondari na shule moja ya msingi wilayani Ilala.

Shule zilizoshiriki mdahalo huo ni Shule za Sekondari Misitu na Kerezange na Shule ya Msingi Misitu.

Akiongoza mdahalo huo, Mwenyekiti wa Kituo cha Taarifa na Maarifa, Zahara Omary alisema matukio ya ukeketaji yanaendelea na kwa Desemba mwaka jana walifanikiwa kuokoa watoto watatu maeneo ya Kivule.

"Tulipata taarifa mzazi alitaka kuwakeketa watoto wake watatu, tulifanikiwa kuwatorosha watoto hao ambapo mmoja alikuwa katika hatua ya mwisho ya kuandaliwa ili ngariba aanze kumkeketa," alisema.

Aliongeza kuwa waliwaweka chini ya uangalizi na baadaye waliwasiliana na wazazi na taratibu zilifuatwa watoto wakarudishwa nyumbani.

Wanafunzi, wakichangia kwa nyakati tofauti na kwa masharti ya kutoandikwa majina yao, walisema wapo baadhi ya mabinti wanafanyiwa ukeketaji kwa lengo la kupata zawadi, zikiwamo fedha.

"Nilimwambia jirani yetu 'toroka usikeketwe', akanijibu 'weeeee siwezi kutoroka, mama ameniandalia zawadi nyingi na fedha nitatunzwa," alidai binti huyo.

Alisema kuna wazazi wanahitaji kupewa elimu ili waache kudumisha mila hizo kwa kuwa inaonyesha elimu inayotolewa haijawafikia.

Wanafunzi wengine walidai wapo wenzao waliokeketwa na waliamua kuacha shule na baadhi walipata ujauzito kwa kuwa baada ya matukio hayo, huaminishwa kwamba wamekuwa wakubwa na wanaweza kufanya jambo lolote.

Katika maombi ya jumla, wanafunzi hao walisisitiza elimu zaidi itolewe, ikiwezekana nyumba kwa nyumba kwa kuwa katika familia zao, wanaona hizo mila bado zipo na kuziacha inaonekana ni kama kosa kubwa.


PRICEWATERHOUSECOOPERS SERVICES LIMITED
Cheti cha usajili namba 34477
Sheria ya makampuni, 2002
(KIFUNGU 334 (1))

MAAMUZI YA HIARI YA WANAHISA KUFUNGA KAMPUNI

Umma unafahamishwa kuwa katika kikao cha PricewaterhouseCoopers Services Limited (kampuni), yenye usajili namba 34477, kilichofanyika tarehe 18 Januari 2023 mazimio maalumu yafuatayo yalipitishwa:

1. Kufuatana na kifungu 331 (1) (b) cha Sheria ya Makampuni ya 2002, kuwa kampuni ifutwe kwa hiari; na
2. Wanahisa wamemteua Joseph Lyimo wa Pemba House, 369 Toure Drive, Oyster Bay, S.L.P 45, Dar es Salaam, Tanzania kuwa mfilisi wa kampuni.

Umma na wahusika wanafahamishwa kupeleka madai yao kwa usaili ndani ya siku thelathini (30). Maombi yote yatayopelekwa baada ya siku 30 kuisha hayataandikishwa.

JOSEPH LYIMO
MFILISI wa PRICEWATERHOUSECOOPERS SERVICES LIMITED

217266202

# Samia aridhia eneo Magereza kumegwa ili wapewe wananchi

**Na Jenifer Gilla**

RAIS Samia Suluhu Hassan amemaliza mgogoro wa ardhi yenye ukubwa wa ekari 7,495.74 uliodumu kwa zaidi ya miongo mitatu kati ya vijiji vya Kata ya Kingale, Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa na Gereza la King'ang'a.

Mgogoro huo umetatuliwa baada ya kiongozi huyo kuagiza eneo lenye ukubwa wa ekari 3,272.4 libaki kwa wananchi kwa shughuli za kilimo, mifugo na kiuchumi na eneo lililobaki lichukuliwe na Magereza.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, aliwasilisha jana taarifa hiyo kwa niaba ya Rais Samia mbele ya wananchi na viongozi wa kata hiyo ambayo ardhi yake inasifika kuwa na rutuba inayofaa kwa shughuli za uzalishaji.

"Ardhi yote ni mali ya serikali, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi alipofika hapa alifikisha hili jambo kwa Mheshimiwa Rais aamue na Rais Samia ametoa suluhu kwa Wanakingale," alisema Senyamule.

Alisema Rais Samia ameagiza ndani ya mwezi mmoja, watu wa ardhi waonyeshe utaratibu wa maeneo yaliyogawanywa, yapimwe na kuweka alama zinazoonekana kwa kila mmoja.

Vilevile, aliwasihi wanavijiji na Magereza kutunza mipaka na kuzuia mwingiliano wa matumizi kwa kuwa wananchi wapo upande wa Bonde linalofaa kwa umwagiliaji.

"Wizara ya Kilimo mfanye utaratibu wa kujenga mabwawa kwa ajili ya umwagiliaji na mifugo pia, mjenge majosho kwa ajili ya kuosha mifugo ya wananchi," aliagiza Senyamule.

Mkuu wa Mkoa aliwataka wananchi na Magereza kutumia fursa hiyo na miundombinu itakayojengwa kufanya shughuli zenye kuleta maendeleo.

Mbunge wa Kondoa Mjini, Ally Makoa, alimshukuru Rais Samia kwa uamuzi alioufanya kuwa umefuata mapendekezo waliyoyatoa kwake ya kupatiwa eneo kutoka kwenye mpaka wa Magereza.

Vilevile, Ally alimshukuru Rais Samia kwa kuwapelekea wataalamu kutoka wizarani kwa ajili ya kujenga miundombinu kwenye eneo hilo.



Naibu Spika na Mbunge wa Jimbo la Ilala, Mussa Zungu (kushoto), akiwa na viongozi wa CCM Kata ya Kivukoni jijini Dar-es-Salaam wakikata keki baada ya matembezi ya kuadhimisha miaka 46 ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) juzi. Wengine ni Mwenyekiti wa CCM Dar es Salaam, Abbas Mtemvu, Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Ilala, Said Side na Diwani wa Kata ya Kivukoni, Sharik Choughule na wadau wengine. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Katibu TUICO: Nilijengewa nyumba na chama kama zawadi

**Na Grace Gurisha**

KATIBU Mkuu wa Chama cha Wafanyakazi wa Viwanda, Biashara na Taasisi za Fedha na Huduma (TUICO), Boniface Nkakatisi, ameieleza mahakama kuwa alijengewa nyumba na chama hicho kama zawadi kutokana na utendaji bora wa kazi tangu mwaka 1996.

Pia amedai aliitwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kwa ajili ya kuhojiwa kuhusu nyumba aliyojengewa na TUICO eneo la Mwanagati, Wilaya ya Ilala, Dar es Salaam kwa madai kuwa kuna ubadhirifu umefanyika.

Nkakatisi alidai hayo mbele ya Hakimu Mkazi Rehema Liana wa Mahakama ya Wilaya Ilala iliyoko Kinyerezi, Dar es Salaam wakati akitoa ushahidi wake katika kesi ya madai aliyofungua dhidi ya alikuwa Mwenyekiti TUICO Tawi la TANESCO, Mambo Mkufu. Nkakatisi alidai Baraza Kuu la Taifa la TUICO lilifikia uamuzi wa kumjengea nyumba na sio kwa sababu ya kustaafu kama alivyodai Mkufu kwa kuwa yeye hajawahi kustaafu, hivyo alijengewa kama zawadi.

"Kujengewa nyumba hii ni kama zawadi kwa sababu nilikiinua chama kutoka chini kabisa hadi kilipofikia sasa. Hakuna ubadhirifu wowote kwenye hii nyumba, TAKUKURU waliniita mara nyingi kunihoji, lakini hawakuletewa taarifa hizo, walipewa na nani?" Nkakatisi alidai.

Nkakatisi alidai alijua kama Mkufu ndiye alipeleka taarifa za nyumba TAKUKURU kwa kuwa wakati anazungumza na vyombo vya habari, alidai taarifa hizo atazipeleka huko na pia tangu mwaka 1996 hajawahi kupata tatizo lolote kazini.

Alidai aliomba alipwe fidia kwa sababu alikashifiwa, alivunjiwa heshima, wanachama wamekuwa na hofu juu yake kutokana na fedha zao na pia hata familia yake imekuwa ikimuuliza maswali juu ya tukio hilo.

Pia alidai Mkufu alipeleka taarifa hizo Wizara ya Kazi, Shirika la Umeme (TANESCO) na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA), akidai kuwa kuna ubadhirifu amefanya ikiwamo kuvunja katiba ya chama hicho.

Akijibu maswali ya upande wa mdaiwa (Mkufu), Nkakatisi alidai amefika mahakamani kwa gari la ofisi kwa kuwa yeye ni Katibu Mkuu wa chama hicho na pia shauri hilo sio lake binafsi, bali pia la chama hicho.

Shauri hilo limeahirishwa hadi Februari 13, 2023 kwa ajili ya kuendelea kusikilizwa kwa mashahidi wa upande wa Nkakatisi.

Nkakatisi alifungua kesi ya madai namba 79, 2021 dhidi ya Mkufu, akiomba mahakama imwamuru alimpe fidia ya Sh. milioni 200 na pia amwombe radhi kwa kumkashifu.

## Kamati ya Bunge yashtuka matumizi wahamiaji haramu

**Na Romana Mallya,** DODOMA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama imesema kila mwaka serikali inatumia Sh. bilioni 5.67 kuwatunza wahamiaji haramu magerezani kiasi ambacho kingeweza kununua madawati 81,030.

Mwenyekiti wake, Vita Kawawa, akisoma taarifa ya mwaka ya shughuli za kamati hiyo jana bungeni jijini hapo, alisema taarifa za wizara inaonyesha katika kipindi cha Septemba hadi Desemba 2022, jumla ya wahamiaji haramu 7,493 walikamatwa maeneo mbalimbali.

"Uchambuzi uliofanywa na kamati, ulibaini kuwa katika kipindi cha Septemba hadi Desemba mwaka 2022, katika magereza mbalimbali kulikuwa na wafungwa na mahabusu wahamiaji haramu wapatao 3,108.

"Idadi hii imeongezeka kwa asilimia 93 kulinganishwa na wahamiaji haramu 1,608 waliokuwapo magerezani katika kipindi kama hicho mwaka 2021.

"Kuwapo kwao magerezani kunaigharimu serikali wastani wa Sh. 15,540,000 kwa siku katika kuwapa huduma mbalimbali za msingi," alifafanua.

Alisema ikiwa hali hiyo itabaki kama ilivyo, serikali itakuwa inatumia Sh. bilioni 5.67 kwa mwaka kuwatunza wafungwa na mahabusu hao.

"Kiasi hiki kingeweza kununua madawati 81,030 kwa kila dawati Sh. 70,000, Bunge linaazimia serikali ije na mpango mkakati wa muda mrefu unaotekelezeka kuhakikisha nchi haiendelei kuwa na wahamiaji haramu," alisema.

Akichangia hoja hiyo, Mbunge wa Viti Maalum, Felister Njau alisema waliomba kuwapo mkakati wa kuondoa wahamiaji haramu nchini.

Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Fakharia Shomar Khamis alisema suala la wahamiaji haramu ni zito kwa kuwa linaongeza msongamano magerezani.

"Kuna mtazamo wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwamba kama wameingia kisheria wanawagongea wapite waende zao au amekuja kinyume cha kisheria anaambiwa arejee kwao, kuwalisha magerezani mtu kakaa akiondoka kama alikuja na lishe duni, anaondoka ametengemaa Tanzania," alisema.

**HABARI KITAIFA**

# Ilivyozikwa miili ya ndugu 12 wa ajali

**Na Waandishi Wetu**

SIMANZI ilitawala jana kwa mamia ya wakazi na wageni kwenye Kijiji cha Kurungu, Kata ya Kelamfua Mokala wilayani Rombo mkoani Kilimanjaro wakati miili 12 ya ndugu wa ukoo wa Mrema ilipofikishwa kwenye makaburi ya familia hiyo kwa ajili ya maziko.

Kabla ya wanavijiji kugawana maeneo ya kuwapumzisha ndugu hao, ibada ya pamoja ya maziko yao ilifanyika kuanzia saa 2:47 asubuhi kwenye viwanja vya Hospitali Teule ya Huruma inayomilikiwa na Kanisa Katoliki.

Ukimya ulitawala kwa wakati wote huku baadhi ya watu wakipoteza fahamu wakati miili hiyo ikiteremshwa kwenye magari na kuwekwa kwenye eneo la wazi.

Katika familia ya Athanas Mrema, ambako kulikuwa na makaburi matatu ya baba na wanawe, hali ilikuwa mbaya zaidi kwa watu kuzimia kwa kukosa hewa kutokana na msongamano mkubwa wa watu waliojitokeza kushuhudia maziko hayo.

Hata hivyo, mwili wa Athanas Mrema haukuingizwa eneo la ibada na uliondolewa haraka kupelekwa nyumbani, kukiwa na maelezo kuwa ulikuwa umeharibika.

Misa takatifu kwa ajili ya kuwaombea ndugu hao wa familia ya ukoo wa Mrema, iliongozwa na Msaidizi wa Askofu wa Jimbo Katoliki Moshi, Padri Deogratias Matiika, aliyewataka wanafamilia wa ukoo wa Mrema waliobaki kuendelea kumtegemea Mungu, huku akiwataka kuacha kusafiri wakiwa pamoja au kutumia chombo kimoja.

**SERIKALI YATOA UBANI**

Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Omari Mgumba alisema serikali imetoa Sh. milioni nne kama 'ubani' kwa familia za ndugu waliopoteza maisha katika ajali hiyo.

Alisema licha ya serikali kugharamia msiba huo kwa kusafirisha miili kufika kwenye familia zao mkoani Kilimanjaro, pia imetoa fedha hizo kama sehemu ya kuwafariji wafiwa.

**MADEREVA WAKOROFI**

Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, akitoa salamu za serikali katika maziko hayo, alisema: "Madereva, kazi ya udereva ni taaluma kama zilivyo taaluma zingine. Mnapobeba watu au mizigo, ni lazima mfuate sheria, tumeweka vibao lakini hamwelewi. Mnatupa shida sana na matokeo yake ni haya ya kupoteza maisha ya watu wasio na hatia."

**MAJERUHI WAIMARIKA**

Majeruhi watano kati ya 10 waliokuwa wamelazwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Tanga (Bombo) wanaendelea kuimarika taratibu baada ya kufanyiwa upasuaji.

Akizungumzia maendeleo ya majeruhi hao, Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Bombo, Dk. Naima Yusuph, alisema wagonjwa hao waliobakia kwenye hospitali hiyo, wanaendelea vizuri kiafya.

Ajali hiyo iliyopoteza ndugu 16 wa familia moja, ilitokea usiku wa Februari 3 mwaka huu eneo la Magira Gereza, Wilaya ya Korogwe mkoani Tanga barabara ya Segera/Buiko.

Ilitokea baada ya lori la mizigo aina ya Mitsubishi Fusso lenye namba za usajili T 673 CUC kugongana uso kwa uso na basi dogo aina ya Toyota Coaster lenye namba T 863 DXN (Special Hire).

Basi hilo lilikuwa limebeba mwili wa marehemu Athanas uliokuwa unasafirishwa kutoka Dar es Salaam kwenda Rombo kwa ajili ya maziko, likiwa na waombolezaji 26.

Ndugu wa familia moja waliofariki dunia kwenye ajali hiyo ni Nestory Athanas, Doris Mrema, Tony Mrema, Athanas Mrema, Augustino Mrema na Eveline Mrema.

Wengine ni Kennedy Mrema, Godwin Mrema, Zawadi Mrema, Elizabeth Mrema, Julieth Mrema, Cosmas Mrema na Rajab Mrema.

Wengine ni Rozina Lamosa, Festo Ndunguru, Yussuf Saimon, Eluminata Silayo na Festo Mwambungu.

***Imeandikwa: Mary Mosha na Godfrey Mushi (ROMBO) na Oscar Assenga (TANGA)**



Majeneza yenye miili ya waliopata ajali eneo la Korogwe mkoani Tanga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## NOTISI / TANGAZO

**LEGENDS AUCTION MART LTD, DESTENI COMPANY LIMITED, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,HEDANE ENTERPRISES LTD, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS, JY AUCTIONEERS CO.LTD, NGOMENI AUCTION MART, REAL MASTER LTD,DRM AUCTIONEERS & CO.LTD, MAS AND ASSOCIATES CO.LTD,MELVA INTERNATIONAL LTD ,YONO AUCTION MART &CO.LTD ,YARDLEY RECOVERIES AUCTION LTD, SUMA JKT AUCTION MART COMPANY LTD,MAJEMBE AUCTION MART LTD, MABUNDA AUCTIONEER MART CO.LTD** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muunganowa Tanzania, chini ya Benki ya **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC,** tunatoa notisi ya kulipa deni kwa mdaiwa ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| MWANZA | SAMSON JOSEPH KASHEKU | 1.NYUMBA YENYE HATI NA. 43118 LR MWANZA KIWANJA NAMBA 1535, KITALU 'A' NORTH BUSWELU ,KWA JINA LA JOSEPH LWIZA KASHEKU. 2.NYUMBA YENYE HATI NA. 52751 LR MWANZA KIWANJA NA. 973/1, KITALU 'B' NYEGEZI KWA JINA LA SAMSON JOSEPH KASHEKU 3.NYUMBA YENYE HATI NA. 52750LR MWANZA ILIYOPO KWENYE KIWANJA NA. 971/1, KITALU 'B' NYEGEZI KWA JINA LA JOSEPH LWIZA KASHEKU 4. NYUMBA YENYE HATI NA. 50140 LR MWANZA ILIYOPO KWENYE KIWANJA NA. 164, KITALU ' J' NORTH BUSWELU KWA JINA LA ZACHARIA MABULA KISUMO | 1.JOSEPH LWIZA KASHEKU 2.SAMSON JOSEPH KASHEKU 3.JOSEPH LWIZA KASHEKU 4.ZACHARIA MABULA KISUMO | 1.NORTH BUSWELU -MWANZA 2.NYEGEZI MWANZA 3.NYEGEZI MWANZA 4.NORTH BUSWELU-MWANZA | 21/02/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | SAIDI AKILIMALI KALILWA | NYUMBA | SAIDI AKILIMALI KALILWA | MWASONGA KIGAMBONI | 14/02/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MAIN | CHEX ENGINEERING LTD | NYUMBA ILIYOPO KWENYE KIWANJA NAMBA 110 KITALU '15' NA HATI NAMBA 69065 | CHEDIEL GASPER MSHANA | BUNJU-KINONDONI | 11/02/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| AGGREY | MPOKI BROWN MWAIPASI | NYUMBA (2) | MPOKI BROWN MWAIPASI | 1.GONGOLAMBOTO 2. KILUVYA | 22/02/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| HEAD OFFICE | EVELYNE KASHUSHURA MHINA | GARI TOYOTA SPACIO NO.T973 CKU | EVELYNE KASHUSHURA MHINA | CHANG'OMBE TEMEKE | 10/02/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | FAISAL SALUM HASSAN | GARI T396 DJR HINO RAINBOW | FAISAL SALUM HASSAN | TEMEKE | 15/02/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | FELISTA MATOKE NYANGWE | NYUMBA YENYE HATI NA.45634,KIWANJA NA.183 KITALU 'B' | SOPHIA KIBOKO CHACHA | KISEKE-MWANZA | 15/02/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MAIN | JOYCE GENES SHIRIMA | NYUMBA | FRIDA ELIESKIA FUE | HONDOGO KIBAMBA | 21/02/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TANDALE | MARYAN GENERAL SUPPLIES | NYUMBA | MARYAN KAPAMA | KIMARA | 16/02/2023 SAA 12:00 MCHANA NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UBUNGO | FAUSTIN JOSEPH MWACHA | NYUMBA | FAUSTIN JOSEPH MWACHA | GOBA MATOSA | 15/02/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TANDALE | HAMAD ABDALLA MNEMBWE | NYUMBA | HAMAD ABDALLA MNEMBWE | TANDALE | 14/02/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | HAJI HARAMBE BIBOZE | NYUMBA | HAJI HARAMBE BIBOZE | VIKINDU MASHARIKI | 17/02/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| AGGREY | LILIAN CLAUDY KANJE | NYUMBA YENYE HATI NAMBA 145001 | LILIAN CLAUDY KANJE | KIGOGO- MANISPAA YA KINONDONI | 22/02/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MAIN | KWANZA KILWAMINING & PRODUCTS LTD | NYUMBA YENYE HATI NA.94894,KIWANJA NA.460 KITALU '47' | MWALIMU ALLY ZUBERY | KIJITONYAMA | 24/02/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBEYA | KIVAULA MLIMKA LUHANGA | NYUMBA (2) ZENYE HATI MILIKI | KIVAULA MLIMKA LUHANGA | 1.MBEYA MJINI 2. TUNDUMA | 16/02/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | VENANCE JISKAKA MWAKYABALA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | VENANCE JISKAKA MWAKYABALA | MWANJELWA , MBEYA MJINI | 17/02/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | ROGIMWA AGRO COMPANY LIMITED | KIWANJA CHENYE HATI NAMBA 083KYL/1204 | ROGGERS GIDION MWAMENGO NA ANNA DANIEL SANGA | ITETE KYELA MBEYA | 21/02/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | UYACODE VICOBA PROGRAM | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI KNDO 29299-KND/MBR/MWZ/10/2 | UYACODE VICOBA PROGRAM HQ | MAKUBURI UBUNGO | 21/02/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | JUMANNE MOHAMED KAPOLI | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | MATHIAS CHARLES NDETTO | KISESA-MWANZA | 16/02/2023 SAA 12:00 MCHANA NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | HASSAN BUGANDA KAPOJONGO | NYUMBA | HASSAN BUGANDA KAPOJONGO | USTAWI-MWANZA | 15/02/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | MARTINA CORRONATUS RYOBA | 1.NYUMBA 2. KIWANJA | MARTINA CORRONATUS RYOBA | IGELEGELE BUGARIKA NA BUJINGWA-MWANZA | 14/02/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | DICKSON ANICETH GREEN | NYUMBA | DICKSON ANICETH GREEN | LUKOBE-MWANZA | 21/02/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | JOSEPH KIGONGO IBAMBASI | NYUMBA | JOSEPH IGONGO IBAMBASI | NYAKATO-MWANZA | 16/02/2023 SAA 12:00 MCHANA NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | MANGWE EMMAUEL WAMBURA | VIWANJA VIWILI VYENYE HATI MILIKI | MANGWE EMMANUEL WAMBURA | ILALILA-MWANZA | 15/02/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | CHRISTOPHER MANGARAYA WAMBURA | KIWANJA | CHRISTOPHER MANGARAYA WAMBURA | BUJINGWA-MWANZA | 14/02/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | KIPEJA TIMBER AND GENERAL SUPPLIES | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | JOHN TIMOTH PANGANI | IGOMA-MWANZA | 17/02/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | ABAS HAMAD ISSA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | PETER NDULU MAHARAGE | MISUNGWI-MWANZA | 16/02/2023 SAA 12:00 MCHANA NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| ILALA | NICKSON LUDOVIC MTALEMWA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI NA.84704 | NICKSON LUDOVIC MTALEMWA | MAJOHE | 21/02/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ILALA | BIAGATI SEA FOODS CO. LTD | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NAMBA TMK033735 | DAVID ABEL MLAU | CHARAMBE -MBAGALA | 21/02/2023 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| DODOMA | BENEDICTO WILSON MAGAYA | NYUMBA | BENEDICTO WILSON MAGAYA | NZUGUNI -DODOMA | 22/02/2023 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | LEAH JOHN MPAPALIKA | NYUMBA | LEAH JOHN MPAPALIKA | KIMARA-STOPOVER | 21/02/2023 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1 Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba, Kiwanja,Gari au Shamba ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14

2 Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali,hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.

3 Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no.**0715868000/0765999000/0714939933/0655715138/0714208208/0719351040**

4 Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba Benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi Benki bila gharama yeyote.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hili la ajali, kila mmoja sasa awajibike kwa nafasi yake

**NI** kila wakati umma haupumziki, simulizi za kuumiza, ajali kila wakati. Kwa mpito wa wikiendi hii simanzi zinatawala mkoani Tanga, hata kitaifa wanafamilia waliokuwa safarini kumpumzisha mpendwa wao mkoani Kilimanjaro, wakitokea Dar es Salaam, nao yamewakuta kwa pamoja.

Kinachoumiza sana ni pale wanandugu hao waliokuwa wanamsindikiza mzee wao wakampumzishe, nao wakaangukia wasifu huo wa kuitwa marehemu; wote wana unasaba wa karibu sana.

Unapowauliza wenye dhamana kuu wa Polisi Kitengo cha Usalama Barabarani, maarufu kwa jina la Trafiki, nao wana malalamiko yao kuhusiana na hizo ajali zinavyowaweka kuwajibika na ulingo huo wa huzuni.

Wanakadiria asilimia 75 za ajali nchini zinatokana na uzembe wa madereva barabarani. Taarifa ya awali ni hata kilichojiri kwa wapendwa wa Tanga na baadhi yao waliwekwa kwenye nyumba ya milele, huko wilayani Rombo, Kilimanjaro jana, kisa ni nidhamu ya udereva.

Hasara ya ajali hizo ni zaidi ya madhara binafsi kiafya kwa wahusika ikiwamo ulemavu wa kudumu na mengine. Hapo hapo watu hao wanahudumiwa, hata kuangukia gharama kubwa maradufu.

Upo wakati mhusika anagharamia, pia anapokosa wa kumgharamia, hospitali husika hubeba mzigo kwa sura pana. Kama ilivyo kawaida ya matibabu hospitali nyingi na hasa za umma, huwajibika na kumhudumia mgonjwa kwanza na suala la malipo huwa linafuata.

Maana yake ni kwamba, hospitali inakuwa sehemu ya dhamana kumhudumia mgonjwa atakapokwama gharama, awe hai au inapotokea katangulia mbele ya haki.

Ni hivi karibuni tulifahamishwa kwamba ili kufanyia uchunguzi mwili wa aliyefariki dunia katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), inagharimu Sh. 250,000 kwa kila mwili.

Sasa katika mikasa ya vifo pale hospitali inapatiwa miili mingi ya kufanyia uchunguzi wa kutolea ripoti na pale haitagundulíwa ndugu na jamaa, dhamana ya gharama inabaki kwa mamlaka ya hospitali.

Kwa ujumla kuna hali ya kwamba kule barabarani kuna shida inayobeba sura zote, nidhamu na uwezo mdogo wa kumudu njia.

Tunajua kuna mengi sana yamefanyika kukabili hali hiyo kwa muda sasa, hata mamlaka husika na hasa polisi trafiki wako katika wakati mgumu.

Ulianzishwa utaratibu wa mafunzo kwa madereva katika Vyuo vya Elimu ya Ufundi (VETA) nchini, pia Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), Dar es Salaam, madereva wananolewa, lakini bado ni mtihani, ajali mbaya tunazidi kuzisikia.

Tuseme kuanzia usimamizi wa juu kiserikali, wakala wao barabarani polisi, madereva, abiria, wapitanjia na kila mtu anawajibika kwa maana hakuna hata mmoja aliye salama na ajali barabarani, kwamba haimgusi.

Ni kila mtu kwa nafasi yake anafaa kuchangia kukabili haya yanayotuondolea uhai kwa mpigo, kama kilichotokea mkoani Tanga mwishoni mwa wiki.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Jenifer Gilla

## Muungwana Lazima Nilonge

# Ziro ukeketaji ikate mila zinazochochea

**TANZANIA** na mataifa mengine inapiga kampeni ya 'ziro kwa ukeketaji' na inaungana na nchi nyingine kuadhimisha Siku ya Kimataifa ya Kutovumilia Ukeketaji.

Mwaka huu kauli mbiu inakumbusha ushirikiano na wanaume na wavulana kubadilisha mifumo ya kijamii na jinsia ili kutokomeza ukeketaji.

Kwa mujibu wa Shirika la Afya la Umoja wa Mataifa (WHO) zaidi ya wanawake na wasichana milioni 200 wamefanyiwa ukeketaji jambo ambalo halikubaliki kwa kuwa ni kinyume na haki za binadamu.

Ingawa kumefanyika juhudi kubwa kupunguza ukatili huo, bado inakadiriwa wasichana na wanawake 3,000,000 wako katika hatari ya kukeketwa kila mwaka na Tanzania imo kwenye hatari.

Kwa mujibu wa utafiti wa Kidemografia na Afya Tanzania wa mwaka 2015/16 Manyara ndio mkoa unaoongoza kwa ukeketaji nchini kwa asilimia 58 ikifuatiwa na Arusha yenye asilimia 47 na Mara 41.

Aidha, utafiti huo pia unaonyesha kuwa mwanamke mmoja kati ya 10 nchini amekeketwa ukiongezeka kulingana na umri. Asilimia 19 ya wanawake wenye umri wa miaka kati ya 45 hadi 49 walikuwa wamekeketwa ukilinganisha na asilimia 5 ya wanawake wenye umri kati ya miaka 15 hadi 19.

Utafiti huo unadhihirisha kuwa bado kuna kazi kubwa ya kufanya ili kutokomeza vitendo hivyo ikiwamo kuwekeza zaidi kwenye elimu kwa kuwa unaonyesha wanawake wenye elimu ya sekondari wana uelewa mkubwa zaidi kuhusu athari za ukatili kwa asilimia 97 ukilinganisha na wanawake ambao hawakufikia ngazi ya elimu ya sekondari kwa asilimia 71.

Kwa mantiki hiyo kuna haja ya serikali pamoja na wadau wa haki za wanawake na binadamu kwa ujumla kuangalia ni wapi wamekosea katika suala zima la kutoa elimu kwa jamii kwa kuwa linaonekana bado halijazaa matunda.

Katika maadhimisho ya siku hiyo WHO inatoa rai kwa wadau wanaohusika katika kukomesha ukeketaji kusherehekea mafanikio, kutetea kuachana na mila na desturi hiyo na kuongeza uelewa.

Kuna haja ya kutoa elimu kwenye jamii zinazoshamiri vitendo hivyo, ili wazitambue mila na desturi mbaya zinazochangia kuwapo kwa vitendo hivyo kwa kuwa ukeketaji kwa baadhi ya makabila ni sehemu ya utamaduni hivyo si rahisi kuumaliza bila jamii yenyewe kwa hiyari yao kuamua kuachana nao.

Lakini kuwaelimisha wale ambao wamepitia kadhia hiyo ili wawe mstari wa mbele kukemea kwa kuelezea madhara wanayoyapata baada ya kufanyiwa ukatili huo kwa kuwa ripoti inaonyesha asilimia 86 ya wanawake waliokeketwa hawakubaliani na kitendo hicho na wanatamani kisiwepo kabisa.

Kuna haja ya kuongeza nguvu katika kuwasaka na kuwaelimisha mangariba ambao kuwapo kwao kunashawishi kuendelea kushamiri kwa vitendo hivyo, wapewe elimu pamoja na kuwawezesha kiuchumi ili waachane na vitendo hivyo.

Vilevile kuna haja ya serikali kuyaunga mkono mashirika yasiyo ya kiserikali yanayofanya kazi kubwa ya kukemea vitendo ili kuwaongezea nguvu ya kupambana kwa kuwa peke yao hawawezi, watu hawa wanafika maeneo ambayo wakati mwingine serikali haiwezi kufika.

Pia kuwapo na sheria kali inayojitegemea inayokemea vitendo vya ukeketaji ili kuongeza uzito katika suala hilo kwa kuwa inaonekana kuwa sheria zilizopo misumeno yake sio mikali sana ndio maana vitendo vinaendelea kufanyika licha ya maonyo ya serikali.

Moja ya madhara wanayopata wanawake waliokeketwa ni vifo vinavyotokana na kutokwa na damu muda mrefu, maambukizi, maumivu ya muda mrefu, huzuni na utasa.

## Wafanyabiashara walalama kukithiri majitaka sokoni

**Na Beatrice Shayo**

WAFANYABIASHARA wa Soko la Bombom, Kiwalani wilayani Ilala jijini Dar es Salaam wamelalamika kufanya shughuli zao kwenye mazingira magumu kutokana na kusambaa kwa maji machafu ya chooni licha ya kwamba wanalipa ushuruku kila siku.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, wafanyabiashara hao, akiwamo Mashaka Mgugule, walidai majitaka yanapojaa huingia kwenye maeneo wanakofanyia biashara na hivyo kuweka hatarini usalama wa afya yao.

"Hili soko baada ya kulalamika tukawekewa sehemu ya kuoshea bidhaa, lakini hazina ubora maana chemba ya kuoshea vitu vya kula inaingia katika chemba ya choo. Hii inawezekana kweli?

"Haya ndiyo yaliyofanyika katika ujenzi wa hili soko ambalo mwonekano wake ni mzuri. Tunaosha biashara zetu za kula halafu paipu yake inaenda kuungana na chemba ya chooni, ikijaa maji yote yenye kinyesi yanarudi huku tunapofanyia biashara," alilalamika.

Alipaza sauti serikali iangalie uwezekano wa kuboresha mazingira yao ili yafanane na kodi na tozo mbalimbali wanazolipa.

Mbegu Bakari, mfanyabiashara sokoni huko, alisema soko la awali halikuwa na ubora, lakini walilitengeneza mpangilio mzuri kwa kuweka vizimba vyenye marumaru kwa kila mmoja na wakaombwa kuhama ili kuboreshwa zaidi mazingira ya soko hilo.

"Tulivyoambiwa turudi, tulihoji mbona hatujaboreshewa meza zetu kama tulivyoahidiwa? Tunaouza samaki, tukaambiwa 'kama hamtaki tutawaleta watu wengine kutoka sehemu nyingine,'" alidai.

Alisema iliwalazimu kurejea kwenye soko hilo na baada ya miezi miwili wakaambiwa walipe ushuru kwa mwezi yaani wale ambao wametengenezewa wanalipa Sh. 9,000 na wao ambao hawajatengenezewa hata meza, wanalipa Sh. 15,000.

"Tuliuliza 'sisi na wale tuna tofauti gani? Wenzetu wameboreshewa sisi hamjatuboreshea, tukaambiwa kama hamtaki ondokeni hamlazimishwi kufanya biashara, sisi tumeshaamua," alidai Bakari.

Bakari alisema viongozi wamekuwa wakitumia kauli za vitisho, jambo ambalo linawaumiza licha ya kufanya biashara zao kwenye mazingira magumu.

Mwenyekiti wa soko hilo, Mwidini Ndoranga, alisema mazingira ya biashara ni magumu kwa kuwa kuna mifereji ambayo hurejesha kinyesi kwenye maeneo ya biashara na kuziweka hatarini afya zao.

"Wakiosha vyombo, yale maji yanakwenda kwenye chemba ya choo, kule ikijaa yale maji yanarudi kwa walaji ambayo yanakuwa na kinyesi, hii ni changamoto kubwa inayowatesa hawa wafanyabiashara, ndio maana wanalalamika," alisema Ndoranga.

Alisema mkuu wa masoko hajakutana na wafanyabiashara hao ili kujua changamoto ambazo zinawakabili na kuzitatua.




Mkuu wa Kitengo cha Wateja Binafsi na Biashara za Kati wa Benki ya Exim, Andrew Lyimo (wa pili kulia), akizungumza na waandishi wa habari (hawapo pichani) kuhusu hitimisho la kampeni maalum ya benki hiyo inayofahamika 'Chanja Kijanja, Kimasta Zaidi' iliyolenga kuwashawishi wateja wake wanaomiliki kadi za MasterCard kufanya miamala zaidi kwa kutumia kadi hizo jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# 'Mtoto asiporipoti shuleni, mzazi avishwe sare ya shule'

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Singida kimewataka wakuu wa wilaya mkoani hapo kuchukua hatua ya kuwavisha sare wazazi na kuwapeleka shuleni wakasome kwa niaba ya watoto wao ambao hawajaripoti sekondari kuanza kidato cha kwanza hadi sasa.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Singida, Martha Mlata, aliyasema hayo juzi alipozungumza na mamia ya wananchi waliohudhuria maadhimisho ya miaka 46 ya kuzaliwa kwa CCM yaliyofanyika kimkoa kwenye Kata ya Minyughe wilayani Ikungi.

Martha alisema kuwa hivi karibuni alimweleza Mkuu wa Wilaya ya Singida, Paskas Mulagiri, kwamba akiona mtoto hajaripoti shuleni, aende akamchukue baba au mama.

"DC (Mkuu wa Wilaya) Ikungi na mwenyekiti wa chama kama kuna watoto hawajaenda darasani, wewe kachukue wazazi, valisha 'uniform' (sare) peleka darasani ili watoto wabaki nyumbani," aliagiza.

Akizungumzia uchaguzi uliofanyika ndani ya chama, aliwataka wanachama wa chama hicho kuvunja makundi yaliyokuwapo wakati wa uchaguzi kwa kuwa sasa ni nyakati za kufanya kazi na kukijenga chama.

"Uchaguzi umekwisha ndani ya chama, ninaomba kama kuna makundi yoyote yamebaki ndani ya chama kuanzia shina yaishe, hizi ni nyakati za kufanya kazi na kukijenga chama," alisema.

Kuhusu suala la migawanyiko, Martha alisema katika kipindi chake cha uongozi atahakikisha haruhusu migawanyiko yoyote itokee kwa kuwa kuwapo kwayo kunarudisha nyuma maendeleo ya mkoa.

"Yeyote atakayeonekana analeta mitafaruku na migawanyiko CCM, tuna kanuni, nitatumia kanuni kuhakikisha migawanyiko haitokei," alisema.

Mwenyekiti huyo pia alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuruhusu mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa, akisema CCM itaitumia kufanya shughuli za maendeleo na kuelekezana palipo na dosari.

"Ninaomba mikutano ifanyike lakini kuwe na lugha za staha za kumheshimu mtu mwingine, tutumie fursa hii vizuri kulinda amani iliyopo ambayo imelindwa kwa muda mrefu na CCM," alisema.

Mwenyekiti huyo pia aliwaonya wanachama walioanza kampeni mapema kwa kuwataka waache mara moja kuwasumbua wabunge na madiwani, akiwataka wasubiri kipindi cha uchaguzi mkuu 2025. Mbunge wa Singida Magharibi, Elibariki Kingu, alisema serikali ya CCM katika kipindi cha miaka 46 tangu kuzaliwa kwake, imeleta maendeleo mengi jimboni kwake.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa ilani ya uchaguzi kwenye maadhimisho hayo, alisema serikali imefanikiwa kutekeleza ilani hiyo kwa kiwango kikubwa kutokana na kujengwa kwa miradi mbalimbali iliyogharimu mabilioni ya shilingi.

Serukamba alitoa mchanganuo kuwa katika sekta ya afya mkoa wa Singida umepokea Sh. bilioni 23.3 ambazo zimetumika kujenga hospitali, vituo vya afya na zahanati. Serukamba alisema kwa sekta ya elimu, katika kukabiliana na ongezeko la idadi ya wanafunzi, Mkoa wa Singida ulipokea Sh. bilioni 13.4 za mapambano dhidi ya UVIKO 19 ambazo zimetumika kujenga madarasa 330, vyumba 332 kwenye shule shikizi na mabweni.

Kuhusu hali ya upatikanaji wa maji safi na salama, kwa vijijini imefikia asilimia 61.4 na asilimia 78 kwa maeneo ya mjini, miradi yenye thamani ya Sh. bilioni 61.9 inatekelezwa, hadi sasa fedha zilizopokewa ni Sh. bilioni 27.169.

Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Ikungi, Mika Likapakapa, alisema mikutano ya hadhara itumike kuzungumzia mafanikio na maendeleo yaliyopatikana nchini.

Mkuu wa Wilaya ya Ikungi, Thom Apson, alisema CCM ina kila sababu ya kusherehekea miaka 46 tangu kuzaliwa kwake kutokana na mafanikio makubwa yaliyopatikana ndani ya kipindi hicho.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# Wizara yaanika maficho manane ya mauaji nchini

WIZARA ya Mambo ya Ndani ya Nchi imesema matukio ya mauaji na ukatili yanachangiwa kwa kiasi kikubwa na mambo manane, ukiwamo wivu wa mapenzi.

Naibu Waziri wake, Jumanne Sagini alibainisha hayo bungeni jana alipojibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Fatuma Toufiq, aliyetaka kujua mkakati wa serikali kuzuia matukio ya mauaji, kujiua na ukatili ulioikithiri hasa kwa wanawake na watoto, ikizingatiwa baadhi ya watendaji wa makosa hayo wanatoka ndani ya familia.

Sagini, akijibu swali hilo, alisema serikali kupitia Jeshi la Polisi itaendelea kuwakamata watu wanaotenda makosa ya jinai, yakiwamo ya mauaji na ukatili na kuwafikisha mahakamani ili sheria ichukue mkondo wake.

"Uchunguzi wa Jeshi la Polisi unaonyesha kuwa matukio haya kwa kiasi kikubwa yanasababishwa na watu kujichukulia sheria mkononi, imani za ushirikina, wivu wa mapenzi, migogoro ya ardhi, migogoro kwenye ndoa, kugombania mirathi, ulevi na mmomonyoko wa maadili," alisema.

Naibu Waziri huyo alisema serikali kupitia Jeshi la Polisi itaendelea kutekeleza mkakati wa kutoa elimu na mafunzo kwa jamii ili wananchi wafuate sheria za nchi katika kutatua migogoro inayojitokeza au wanapodai haki zao.

"Aidha, wananchi wanaombwa kuwashirikisha viongozi wa kijamii, kimila, kisiasa na kiserikali, wazee au watu maarufu wanaotambulika na kuheshimika ili kuwaasa ipasavyo na hivyo kuepuka kuvunja sheria za nchi," alisema.



Mbunge wa Jimbo la Kilindi, Omari Kigua, akiuliza swali bungeni Dodoma jana kuhusu lini serikali itajenga kituo cha polisi katika Wilaya ya Kilindi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mbunge: Hali ya upatikanaji samaki Ziwa Victoria mbaya

MBUNGE wa Muleba Kusini (CCM), Dk. Oscar Kikoyo, amesema hali ya Ziwa Victoria hususan upatikanaji wa mazao ya samaki ni mbaya huku samaki wazazi wakiwa chini ya asilimia 0.85.

Akiuliza maswali ya nyongeza bungeni jana, mbunge huyo alisema kulingana na viwango takiwa, kwenye ziwa lolote samaki wazazi wanapaswa kuwa kati ya asilimia tatu hadi tano lakini kwa takwimu zilizotolewa na serikali kwenye ziwa hilo, samaki wazazi wapo chini ya asilimia 0.85.

"Upungufu huo hauhusiani na uvuvi haramu? Task forces (vikosi kazi) zipo Ziwa Victoria, hawa wanaotumwa kwenda kufanya kazi ni wasomi lakini hawana weledi wowote na masuala ya uvuvi na matokeo yake wamekuwa wakikamata hizo zana haramu wanawapiga faini zisizo na kanuni wala sheria, baada ya kuwapiga faini wanawarudishia zana haramu, sasa serikali haioni inaendekeza uvuvi haramu?" Alihoji.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, alisema upungufu wa samaki wazazi unahusiana na uvuvi haramu.

"Tumeweka mkakati shirikishi kupitia vyombo vyetu ambao utakwenda kunusuru hali ile kwanza kulinda samaki wazazi na rasilimali nzima, ili kuwa na uendelevu wa rasilimali hii muhimu kwa nchi yetu," alisema.

Naibu Waziri huyo alisema inawezekana kuna maofisa wanaofanya kazi kinyume cha maelekezo ya serikali na watachukua hatua madhubuti kwa wale wanaoharibu operesheni za kulinda rasilimali za nchi.

Awali, katika swali la msingi, mbunge huyo alihoji ni kwa kiwango gani vikosi kazi vimepunguza tatizo la uvuvi haramu kwenye Ziwa Victoria kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita.

Ulega, akijibu swali hilo, alisema katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia 2017/2018 hadi 2019/2020, Kikosi Kazi kilifanya doria na operesheni kwenye maeneo mbalimbali ya ukanda wa Ziwa Victoria.

"Utekelezaji wa doria hizo uliwezesha kukamatwa kwa zana haramu zilizokuwa zikitumika katika shughuli za uvuvi ikiwamo nyavu za makila, makokoro, nyavu za timba (Monofilament) na nyavu za dagaa.

"Pia, vifaa vilivyokuwa vinatumika kwenye uvuvi haramu na utoroshaji wa mazao ya uvuvi ikiwamo injini za boti pamoja na gari," alisema.

Aliongeza kuwa utekelezaji wa doria hizo kwenye maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria uliwezesha kupungua kwa vitendo vya uvuvi haramu, biashara ya samaki wachanga na utoroshaji wa mazao ya uvuvi kwenda nje ya nchi kwa asilimia 80.

## Waliokuwa wafanyakazi ATCL kulipwa mabilioni

SERIKALI imesema katika mwaka huu wa fedha imetenga Sh. bilioni 10 ili kuwalipa waliokuwa wafanyakazi wa Kampuni ya Ndege nchini (ATCL) waliokuwa wanadai kabla ya mwaka 2016, kampuni hiyo ilipofufuliwa.

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Atupele Mwakibete, aliyasema hayo jana bungeni jijini hapo alipojibu maswali ya nyongeza ya Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Angelina Malembeka, aliyetaka kujua mpango wa serikali kuzuia kuzalisha madeni mapya kwa ATCL na idadi ya marubani wazawa kwenye ndege za ATCL.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri huyo alisema tangu mwaka 2016, wafanyakazi wote wamekuwa wakilipwa na hakuna deni jipya.

Alisema idadi ya marubani wa ATCL ni 106. Kati yao, 11 ni wanawake na 95 ni wanaume.

"Hawa wanawake wanarusha ndege za aina zote zilizoko nchini na kati ya hao marubani 106, mmoja tu sio Mtanzania," alibainisha.

Katika swali la msingi, mbunge huyo alihoji ni lini wastaafu wa ATCL watalipwa mafao yao.

Mwakibete, akijibu swali hilo, alisema kabla ya kuanza kwa juhudi za ufufuaji wa ATCL Septemba 2016, kampuni hiyo ilikuwa inakabiliwa na matatizo ya uendeshaji kwa kukosa mtaji, kuwa na ndege mbovu, kushindwa kulipa madeni ya wazabuni na kutowasilisha michango ya wafanyakazi kwa mifuko ya hifadhi ya jamii.

Alisema kuwa baada ya mwaka 2016, ATCL imekuwa inawasilisha michango ya wafanyakazi kwenye mifuko hiyo.

"Kwa kuzingatia uhakiki uliofanyika, ATCL ina madeni ya Sh. bilioni 4.8 yanayotokana na kutowasilisha michango ya wafanyakazi kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii.

"Fedha za kulipa madeni hayo zimetengwa katika bajeti ya mwaka 2022/23, hivyo madeni hayo ya michango ya wafanyakazi kwenye mifuko ya jamii yatalipwa katika mwaka huu wa fedha," aliahidi.




**Habari zote na Augusta Njoji Dodoma**





## Ujenzi mahakama wakwama kisa hati milki

**Na Steven William,** MUHEZA

MRADI wa ujenzi wa mahakama ya kisasa katika eneo la Bwembwera, Wilaya ya Muheza mkoani Tanga, ambao unafadhiliwa na Benki ya Dunia (WB), umesimama kutokana na kile kinachoelezwa ni kukosekana kwa hati ya umiliki wa kiwanja hicho.

Kwa mujibu wa Hakimu Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya hiyo, Lusajo Mutua, ili mradi huo uruhusiwe kuendelea na kupata fedha ni lazima hati hiyo ipatikane.

"Kuna mradi mkubwa wa kujenga mahakama ya kisasa eneo la Bwembwera unaofadhiliwa na Benki ya Dunia umesimama kwa sababu ya kukosekana hati.

"Tunaomba mamlaka husika (Kamishna Msaidizi wa Ardhi na Msajili wa Hati wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi), kuondoa gharama zote na kubaki gharama za hati pekee," alisema.

Kutokana na mkwamo huo, hakimu huyo aliiomba viongozi husika wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza kusaidia kufanikisha upatikanaji wa hati za viwanja vya Mahakama ili waweze kupata miradi mikubwa ya majengo ya kisasa ya mahakama mpya.

Mbali na tatizo hilo, Lusajo, alisema hivi sasa shughuli za mahakama zinaendelea kupitia 'video conference' hata kama mahabusu hawakuletwa mahakamani, ambapo kwa mwaka 2022, walifanikiwa kusikiliza mashauri 80.

Alisema kwa mwaka 2022, kesi zilizosikilizwa katika Mahakama ya Wilaya zilikuwa 257, mahakama za mwanzo 1,132 na hivyo kufanya jumla ya kesi 1,389.

**"Kuna mradi mkubwa wa kujenga mahakama ya kisasa eneo la Bwembwera unaofadhiliwa na Benki ya Dunia umesimama kwa sababu ya kukosekana hati.**

# Watoa tahadhari matumizi 'headphones', visafisha sikio

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

WATAALAMU wa elimu maalum wanaotekeleza mpango wa taifa wa elimu jumuishi kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari, wametoa hadhari kuhusu matumizi mabaya ya 'headphones' na visafisha sikio kama njiti za viberiti, kwamba yanaliweka kundi hilo katika hatari kubwa ya kupata uziwi.

Matumizi ya muda mrefu ya vifaa hivyo yanaelezwa kusababisha madhara makubwa ya usikivu hafifu au kutosikia kabisa.

Mkufunzi Mwandamizi kutoka Chuo Cha Elimu Maalum Patandi, Stanfod Maganza, aliyasema hayo katika Kata ya Kirua, Wilaya ya Siha, mkoani Kilimanjaro, wakati wa utekelezaji wa programu ya ubainishaji wa watu wenye ulemavu shuleni.

Alisema utafiti unaonyesha kuwa waliko kwenye hatari zaidi ni wanafunzi wa sekondari.

Programu ya ubainishaji wa watu wenye ulemavu shuleni na masuala ya ujumuishaji, inaendeshwa na Shirika la Connects Autism Tanzania (CAT).

"Kuna baadhi ya visababishi vinaweza kusababisha mtu kupata tatizo la ulemavu wa uziwi (kusikia); kwa mfano, kama unavyojua wengine wanazaliwa nao na wengine wanapata kulingana na mazingira na mitindo ya maisha ambayo wanaishi nayo.

"Tumekuwa na vijana wengi wanatumia head phones (spika za masikioni) wanaweka mziki mkubwa na kusikiliza asubuhi mpaka jioni. Matumizi ya head phones au ear phones, kwa muda mrefu yanaweza yakasababisha mtu akapata tatizo la usikivu.

Zaidi aliongeza: "Nimewaambia tu walimu mwelewe kwa sababu vijana wetu wengi wa elimu ya sekondari, ndiyo wanatumia sana vifaa hivyo. Tuanze kuwaelimisha kwamba wako hatarini."

Mbali na vifaa hivyo vya kielektroniki, Maganza alisisitiza kuwa pia matumizi ya visafisha masikio, vinaweza kuathiri ngoma ya sikio na mwisho wa siku mtu kupata uziwi.

Alisema wanaopata ulemavu ambao siyo wa kuzaliwa wanaongezeka kwa kasi kila uchao.

Akiitambulisha programu hiyo, Ofisa Mipango wa Connects Autism Tanzania, Grace James, alisema programu hiyo inalenga kuongeza uwezo wa walimu kuwabaini wanafunzi wenye ulemavu wanapokuwa darasani.


"Wanafunzi wenye ulemavu wako shuleni na walimu wengi wanashindwa kuwabaini. Tunawafundisha wakiona kuna wanafunzi wengine ambao wana tabia ambazo hazieleweki, waache kutumia adhabu kama kigezo cha kutatua tatizo.

"Pia tumewafundisha juu ya ujumuishi, kwamba anapokuwa na mwanafunzi mwenye ulemavu shuleni asimtenge kwa sababu ukiwa na ulemavu siyo kwamba hauwezi, bali una uwezo tofauti.

"Wanafunzi wenye ulemavu wana uwezo tofauti, wanafundishika na kama hawafundishiki basi kuna kitu wanachokiweza kwa umahiri zaidi. Mwalimu akimtambua mapema itasaidia kile kipaji chake kikaendelezwa na kusaidia uzalishaji mali wa taifa letu,"alisisitiza.

Aidha, Ofisa Elimu, Elimu Maalum wa Wilaya ya Siha, Joyce Lukiko, alisema walimu wa sekondari hasa wa wilaya hiyo hawana uelewa wa masuala ya wenye ulemavu.

Kutokana na tatizo hilo kwa walimu kushindwa kuwabaini watoto wenye matatizo ya ulemavu, Lukiko ameiomba Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Ofisi ya Rais, TAMISEMI (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa), kuwajengea uwezo zaidi walimu wa sekondari, kupata uelewa kuhusu tatizo hilo shuleni.




Mkurugenzi Mkuu wa TEMDO, Prof. Frederick Kahimba, akitoa maelezo ya mtambo wa kuzalisha sukari uliobuniwa na kutengenezwa na TEMDO kwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Antony Mavunde, alipotembelea Shirika la Uhandisi na Usanifu Mitambo Tanzania (TEMDO). Waziri aliambatana na Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Sukari, Prof. Kenneth Bengusi. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Aitabiria CCM ushindi wa kishindo uchaguzi serikali za mitaa

**Na Mwandishi Wetu,** HAI

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, Maganda Wang'uba, ametabiri kuwa chama hicho kitashinda tena uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka ujao. Amesema ushindi huo utasababishwa na Rais Samia Suluhu Hassan kucheza vizuri karata ya kuruhusu mikutano ya vyama vya siasa.

Akizungumza jana katika Kijiji cha Mtakuja kilichoko Kata ya Kia, wakati wa maadhimisho ya miaka 46 ya kuzaliwa CCM, alisema ushindi huo utachagizwa na kazi maalum ya kutafuta na kufanya uchambuzi makini wa wagombea waaminifu wasio na chembe ya usaliti.

"Tujiimarishe kwa kutafuta wanachama wengi wapya, waaminifu na ambao watagombea uongozi katika uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka 2024.


"Naagiza, viongozi wa ngazi ya wilaya, anzeni sasa kutafuta ufumbuzi wa matatizo mbalimbali yanayoikabili Kata ya Kia, ikiwamo kero ya miundombinu ya barabara. CCM hii ina kazi kubwa ya kusimamia maendeleo kwa ajili ya wananchi.

"Naomba niwaambie wana CCM wenzangu, uchaguzi wa mwakani tutashinda kwa mshikamano na ushirikiano huu. Kila anayetaka kuwa kiongozi, ajitathmini katika uadilifu na uaminifu wa kuwahudumia wananchi," alisema Maganda.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai, Edmund Rutaraka, akizungumza na wananchi wa Kia, alisema serikali imetekeleza miradi mbalimbali ikiwamo miradi ya barabara, afya, elimu na maji kwa ufanisi katika kata hiyo.

Alisema kwa mwaka uliopita jumla ya vyumba saba vya madarasa vimejengwa katika kata hiyo ili kupunguza msongamano darasani pamoja na kuwapunguzia makali wanafunzi kutembea zaidi ya kilomita 10 kufuata masomo shule jirani. Aidha, Mkuu wa Wilaya ya Hai, Amiri Mkalipa, alisema kwa sasa kipaumbele chake ni kutekeleza agizo la Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, alilotaka ushirikishwaji wa sekta binafsi na wafanyabiashara katika upandaji, utunzaji miti pamoja na kuzisihi familia kuongeza juhudi katika upandaji miti na usafi wa mazingira.

Pia alisisitiza kuwa suala la upandaji miti katika maeneo yote ya wilaya hiyo sio la hiari, bali ni la lazima, huku akizihimiza kaya zote, kujiandaa na upandaji miti wakati wa msimu wa mvua za masika.



# Wanne mbaroni tuhuma wizi wa mafuta mradi SGR

**Na Richard Makore,**
MWANZA

JESHI la Polisi mkoani Mwanza linawashikilia watu wanne kwa tuhuma za kuiba vifaa mbalimbali vya mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa (SGR), yakiwamo mafuta ya dizeli lita 850.

Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Mwanza, Wlibroad Mutafungwa aliyasema hayo jana jijini hapo alipozungumza na waandishi wa habari ofisini kwake.

Mutafungwa alisema watu hao walikamatwa katika operesheni iliyoanza Januari 11, mwaka huu hadi juzi walipofanikiwa kuwakamata watu hao.

Alisema katika operesheni hiyo walimkamata Wilbert Constantine (30) mkazi wa Kijiji cha Mantare wilayani Magu akiwa na madumu 55 yenye ujazo wa lita 20 kila moja yakiwa yamefichwa kwenye kibanda nyumbani kwake.

Aliongeza kuwa katika kibanda hicho pia yalikutwa mapipa matatu matupu, mipira ya kuvutia mafuta na keni za kupimia mafuta.

Aidha, alisema juzi katika Kijiji cha Mantale wilayani Kwimba polisi walifanya msako na kukamata madumu 16 yenye mafuta aina ya dizeli lita 320 yaliyokuwa yamefichwa shambani.

Aliongeza kuwa polisi wanamshikilia Pascal Abadala (20) mkazi wa Salawi wilayani Shinyanga kwa tuhuma za kubeba mafuta ya dizeli lita 190 kwenye pikipiki, huku mwingine akikimbia na kutelekeza madumu ya mafuta lita 200.

Alisema mkazi mwingine Mihambo Elias alikamatwa baada ya kukutwa na madumu matupu 10.

Katika msako huo pia polisi walimkamata Stephano Jacob (35), mkazi wa Salawi mkoani Shinyanga kwa kutajwa kwamba ndiye mwenye mzigo aliokamatwa nao Pascal Abdalah.

Kamanda Mutafungwa alisema operesheni hiyo bado inaendelea katika maeneo yote yanayozunguka mradi wa SGR.

Hivyo, Kamanda Mutafungwa aliwaomba wananchi katika maeneo hayo ya mradi kutoa taarifa kuhusu wahalifu wanaoiba vifaa vya SGR ili wakamatwe na kukomesha wizi unaofanywa na watu hao.



Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga, Janeth Magomi, akionyesha madumu yenye mafuta ya dizeli yaliyoibwa kwenye ujenzi wa mradi wa reli ya kisasa (SGR) jana. **PICHA: MARCO MADUHU**

## RC awataka wananchi, viongozi kuwalinda wawekezaji

**Na Titus Mwombeki,**
KAGERA

VIONGOZI pamoja na wananchi mkoani Kagera wameaswa kuwalinda wawekezaji mkoani humo kwa lengo la kuinua uchumi wa mkoa huo.

Rai hiyo ilitolewa jana na Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Albert Chalamila alipotembelea kiwanda cha kukoboa kahawa cha Source of The Nile Commodities kilichoko wilayani Misenyi mkoani Kagera.

Chalamila alisema kumekuwapo na tabia ambazo siyo nzuri zinazofanywa na baadhi ya viongozi pamoja na wananchi wasio waadilifu zenye nia ya kuwakwamisha wawewekezaji mkoani humo.

Hivyo, aliwataka kuachana na tabia hizo kwani zinakwamisha uchumi na maendeleo ya mkoa huo.

"Ukiona unakuwa na wawekezaji wa namna hii katika wilaya zetu ni kiashiria kuwa mkoa wetu umeanza kuendelea kuna watu wamekuwa na tabia za kukwamisha wawekezaji

Chalamila alieleza baadhi ya faida za kuwapo kwa wawekezaji katika Wilaya ya Misenyi ikiwamo watu kuanzisha miradi itakayosaidia kupata kipato.

"Wapo watu katika wilaya hii walikuwa wanatamani kulima kahawa ila wanajiuliza watapata wapi masoko na ujio wa kiwanda hiki tayari kumefungua milango ya watu kupata soko lao.

Mkurugenzi wa kiwanda hicho, Leonard Kachebonaho, aliishukuru serikali kwa ushirikiano wao kwani imekuwa bega kwa bega naye ili kuhakikisha anafanya kazi katika mazingira rafiki.

Alisema kiwanda hicho kimetoa ajira kwa vijana 45 kutoka wilaya mbalimbali mkoani Kagera.

# Wananchi waiangukia serikali matukio ya mauaji

**Na Restuta Damian,**
BUKOBA

BAADHI ya wakazi wa Manispaa ya Bukoba mkoani Kagera wameiomba serikali kuchukua hatua ikiwamo kuweka mpango wa ulinzi shirikishi kwa ajili ya kuzuia matukio ya mauaji.

Maombi ya wananchi hao yamekuja ikiwa ni siku chache baada ya kutokea mauaji ya watu watatu katika maeneo tofauti ya Manispaa ya Bukoba.

Wakizungumza na Nipashe baadhi ya wananchi hao walisema watu wawili wa familia moja katika Mtaa wa Kyaya, Kata ya Kahororo Manispaa ya Bukoba waliuawa na mwingine aliokotwa mtoni katika Kijiji cha Nkindo Kata ya Kalabagaine Wilaya ya Bukoba.

Mkazi wa Kata ya Kagondo, Audax Kailembo, alisema kwa sasa jamii imeingiwa na hofu kutokana na matukio ya mauaji.

"Nasikitika sana tukio kama hili mtu ameamka asubuhi akafanya shughuli za familia, alimaliza kupandisha watoto kwenye gari waende shule anarudi ndani anauliwa," alisema Kailembo.

"Tena mauaji yenyewe ya kukatwakatwa mwili watu wawili ndani ya familia moja yaani hawaoni huruma ya mama yule kuacha mtoto wa miezi mitano," alisema Kailembo.

Mkazi mwingine wa Kata ya Kashai, Respicus Bwanashamba, alisema matukio ya mauaji yanayoendelea yatawafanya watu kushindwa kufanya shughuli za uzalishaji nyakati za jioni.

Hivyo, aliiomba serikali kuimarisha ulinzi unaoshirikisha jamii nzima ili kufichua na kukomesha vitendo hivyo ambavyo alisema vinaleta picha mbaya kwa Mkoa wa Kagera. Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani mkoani Kagera, Dk. Museleta Nyakiloto alisema majira ya saa 7:00 mchana alipokea miili ya wanawake wawili ambayo ilipelekwa na Jeshi la Polisi. "Miili yao ilikuwa inatoka eneo la Kata ya Kahororo na ilionekana kuwa na majeraha sehemu za shingoni na usoni na ilipokelewa na kuhifadhiwa chumba cha kuhifadhi maiti," alisema Nyakiloto.

Aliongeza kuwa baada ya muda mfupi alipokea mwili mwingine wa mwanamke mtu mzima ukitokea Kijiji cha Nkindo Kata ya Kalabagaine wilayani Bukoba ambao uliokotwa karibu na mto ukiwa na jeraha usoni.




Nipashe

# TESA

Jumanne Februari 7, 2023

TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI




Ukurasa 14

## Iundwe mitaala kufundisha mazingira shuleni na vyuoni

ELIMU

NA PANKRAS LUOGA

IONE HATARI HII

# Mabegi makubwa, mazito kwa mwanafunzi ni kumwandaa...

• Kusagika pingili mgongoni, ubovu wa mabega, shingo, kiuno na miguu



Wanafunzi wakiwa wamebeba mizigo mizito ya vitabu na madaftari wanayoibeba kila siku. **PICHA: MTANDAO**

NI mwanzo wa mwaka wa masomo, shule zimefunguliwa mwezi mmoja sasa. Mambo mengi yanayowasumbua wanafunzi wanaokwenda shuleni kutembea umbali mrefu kuifikia shule na kurudi nyumbani, njaa shuleni hakuna chakula hata maji ya kunywa.

Wanaoishi mijini tatizo la usafiri kwenye mabasi ya daladala na mwendokasi ni changamoto. Lakini pamoja na hayo upo mzigo mgongoni unaowasumbua wanafunzi wa msingi na sekondari ni mabegi makubwa na mazito wanayokukuruka nayo kila siku waendapo shuleni.

Ni mazito na makubwa kama vile wamebeba mawe au vyuma vizito. Tukumbuke bado ni watoto hasa wa shule za msingi ambao wana umri wa chini ya miaka 15, kwa umri wao bado miili yao haijawa imara na kuwa na uwezo wa kunyumbuka na kuhimili mizigo mizito ya kiasi hicho cha kilo hata 15.

Hivyo suala hili linawafanya baadhi ya wanafunzi hao kupata madhara ya kiafya muda mwingine pengine bila hata wao kujua, kwa sababu madhara yake hayatokei kwa siku moja ila baada ya muda mrefu wa kuendelea kubeba mizigo hiyo mikubwa kuliko umri na uwezo wa mwili.

Jamii imekuwa ikishuhudia hayo yote yakitokea katika maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja njiani, barabarani, stendi za mabasi, ya daladala na mwendo kasi jijini Dar Es Salaam lakini bila kuchukua hatua kukabili na changamoto hiyo hasa kwenye mikutano ya wazazi, walezi na uongozi wa shule.

### MADHARA WANAYOPATA

Mabegi hayo yanabeba daftari zote, karatasi, vitabu, kalamu, mikebe, rangi za kuchorea na kwa baadhi ya wanafunzi yana vyakula na vinywaji. Wengine huweka nguo hasa sweta na viatu na sare za michezo.

Nini madhara ya watoto wadogo kubeba mabegi makubwa na mazito kila siku? Athari zipo nyingi hasa kwa watoto wadogo wenye miaka chini ya 18. Baadhi ya athari ni pamoja na kuleta matatizo mbalimbali ya kiafya yanazoweza kujitokeza na kuanza kuonekana katika kipindi kifupi japo nyingi ni baada ya muda mrefu.

Kwa mfano, kupata uchovu wa mwili mzima, kuumwa na mgongo, kusagika kwa pingili za uti wa mgongo, maumivu ya mabega, shingo, kiuno na miguu, kushindwa kusimama vizuri na kupinda mgongo, tatizo la mfumo wa upumuaji, mishipa ya fahamu na kupata matatizo ya msongo wa mawazo.

Madhara haya makubwa ya kiafya yanayotokana na kubeba mizigo mizito mara nyingi si rahisi kutibika.

Pia hutumia muda mwingi sana kuyatibu na fedha nyingi na kuongeza mzigo kwa familia na serikali katika kutoa huduma za kiafya kwa wananchi.

Aidha, watoto hawa hupata usumbufu mkubwa kutokana na kuwa na mizigo mizito muda wote kuanzia nyumbani, kwenye daladala mpaka darasani. Wote ni mashahidi jinsi wanafunzi wenye mabegi makubwa wanavyopata shida kwenye nyombo vya usafiri. Iwe ni kwenye daladala au magari ya mwendo kasi ya lifti na hata kwenye pikipiki. Wakienda darasani nako bado wanaendelea kuteseka na mabegi yao makubwa na mazito.

Zaidi ya hayo yote, utafiti uliofanywa na daktari Muhammad Mushtaq mwaka 2012 kuhusu madhara ya ubebaji wa mabegi mazito kwa wanafunzi wa shule za msingi nchini Pakistani, unaonyesha athari hizo na unataja wanafunzi kufanya vibaya kwenye masomo yao.

Anasema ni kutokana na kushindwa kusikiliza na kufuatilia masomo vizuri darasani kwa sababu za uchovu, kuumwa na mgongo na mabega na msongo wa mawazo ambavyo hufanya mwanafunzi washindwe kutulia.

### UFUMBUZI

Kwanza anashauri kuwa jamii lazima ikubali kuwa mabegi makubwa na mazito kwa watoto ni hatari kwa afya zao sasa na baadaye. Baada ya kulitambua hilo lazima wazazi, jamii, walezi na shule zichukue hatua ya kusaidia watoto hawa dhidi ya changamoto hiyo.

Jamii iwasaidie kwa kuongea na walimu waweke ratiba za masomo ya kila siku ili wanafunzi wachukue daftari chache kulingana na masomo ya siku hiyo. Aidha, ujenzi wa madarasa uangalie kuweka vyumba vya kutunza daftari za wanafunzi kwa kila darasa jipya.

Hili litasaidia wanafunzi kuchukua daftari chache kila siku kuliko iliyo sasa kubeba daftari nyingi kuliko yale yanayohitajika kutumiwa kwa siku hiyo.

Pili wazazi, walezi na familia waongee na watoto wao ambao wanasoma wawafahamishe madhara ya kiafya ya kubeba mizigo kila siku.

INAENDELEA UK.14

# ZAMA ZIMEBADILIKA SANA; TUNATEMBEA NA SimBanking

CRDB BANK
*Tunakusikiliza*

Enzi hizo mzazi akienda benki kuweka au kutoa pesa basi ilikuwa ni lazima ujue. Maandalizi ya kwenda 'mjini' yalikuwa yanaanza usiku mmoja kabla. Kama ni mama basi atakoleza mkaa huku akiimba wimbo wa Bi Kidude kwa sauti ya chini. Atachukua pasi yake ya mkaa na kwenda kunyoosha gauni lake la chui chui halafu atamalizia kwa kufuta vumbi skuna zake nyeusi.

Ilikuwa ni kawaida kuamka asubuhi na mapema kabla ya jogoo la kwanza ili kuwahi siti ya pembeni ya dereva kwenye stendi ya mabasi ambayo ipo takribani kilometa moja kutoka nyumbani na kurudi kwake ni usiku huku akiwa amebeba vifurushi kadha wa kadha. Hakika siku zinaenda!

Miaka takribani 15 baadae baba au mama yule yule akiwa na mvi zake kichwani ana uwezo wa kukaa sebuleni na wajukuu zake wakiangalia taarifa ya habari huku akituma mchango kwenye kikundi chao cha Nia Moja. Umeme ukikatika hata hakasiriki tena kwa nini umeme haujanunuliwa kwa wakati. Ukiwa gizani utamuona akibonyeza simu yake 'twi, twi twi' dakika moja nyingi umeme huooo.

Siku hizi kukatiwa maji bombani utake wewe tu kwa sababu kulipia bili hakuna stress tena. Wale ndugu zangu wapenda mpira au tamthilia hawalalamiki tena kukatiwa matangazo kwa sababu kingámuzi kipo 'full' muda wote. Dada akienda gengeni kuhemea wala habebi bulungutu kwenye kapochi kake ka kijani tena, unaweza kudhani anaenda kumkopa Mangi! Siku hizi kila mtu ameamua kuwa wa kisasa, kwasababu wanatembea na benki mfukoni.



## SimBanking imetufikiria!

Februari 2021, watanzania walipata ahueni ya maisha baada ya benki ya CRDB kuzindua App ya SimBanking iliyoboreshwa zaidi. Bila shaka ubunifu ule ulibadilisha mitazamo ya watu wengi jinsi walivyokuwa wakiichukulia benki.

Eti ilikuwa ni lazima uoge, unyooshe suruali yako halafu ujipulizie na kapafyumu kidogo ndio uende benki. Tumeshatoka huko!

Baada ya Februari 21, watanzania walianza kulipia bili za serikali, tiketi za ndege na mabasi, vingámuzi, bima ya gari na huduma nyingine kadha wa kadha ambazo kwa miaka ya nyuma ilibidi wafunge safari ya kilometa kadhaa.




## Sasa tutaendesha ndinga!

Jumamosi hii baada ya miaka miwili kupita tangu tuanze kulipia bili zetu tukiwa tumejilaza sebuleni kwenye makochi yetu, ghafla tulipigwa na 'surprise' nyingine ya kukata na shoka baada ya kusikia benki yetu ya CRDB imetuandalia zawadi kibao tena kwa mwaka mzima.

Kilicho tuacha hoi ni baada ya kuambiwa kwamba tukiendelea kutumia App yetu pendwa ya SimBanking kufanya miamala tunaweza kuwa miongoni mwa washindi 155,000 wa mkwanja au kuchomoka na moja ya smartphones 200. Kubwa kuliko ni vile ambayo tutaweza kujishindia ndinga mpya aina ya Toyota Crown kila baada ya miezi miwili au Toyota Vanguard ambayo ni zawadi kubwa mwisho wa mwaka. Na si hivyo tu, magari hayo yanakuja yakiwa yamelipiwa bima ya mwaka mzima, mafuta full tanki.

Ni kama watanzania hawakuamini vile mpaka pale walipowaona CRDB wakiwa viwanja wa Zakhiem Mbagala Jumamosi iliyopita wakizindua promosheni ya Benki ni SimBanking huku wakiwashuhudia wasanii wao wapendwa, Nandy, RayVanny, Juma Nature, Sholo Mwamba, MC Kinata, Mzee wa Bwax na Kusah wakilishambulia jukwaa.

Hizi ni Habari njema kwetu sote watanzania ambao tumeamua kubenkika kwenye simu zetu za mkononi kupitia SimBanking App. Wanasema kizuri kula na nduguyo, hivyo ili kuweza kushinda vyote hivi, ni lazima kufungua akaunti kwanza na kisha kujisajili SimBanking.













# Benki ni SimBanking

ELIMU

NA DK. FELICIAN B.KILAHAMA

# Iundwe mitaala kufundisha mazingira shuleni na vyuoni

KWA miaka takribani 40 iliyopita kumekuwapo na mabadiliko makubwa duniani kutokana na 'vitendo hatarishi' hasa katika nchi zilizoendelea.

Pamoja na maendeleo makubwa waliyoyapata shughuli za kiuchumi zimechangia kuiweka dunia 'njiapanda' kutokana na athari zilizojitokeza na kusababisha mabadiliko ya tabianchi.

Kabla ya 'nchi' kuathirika ilikuwa na 'tabia nzuri', watu waliishi maisha bora na ya amani. Mathalani, mvua ya kutosha ilikuwa inanyesha kwa wakati, kulikuwapo vijito, mito midogo na mikubwa ikitiririsha maji mwaka mzima. Uhakika wa kupata mavuno mengi na chakula cha kutosha ulikuwapo.

Ilikuwa nadra kuwapo mafuriko au kusikia madaraja yamezolewa na maji ya mvua au sehemu za makazi ya watu kujaa maji mpaka kuharibu maisha, nyumba na mali.

Hali ya hewa ya sasa inayojulikana kuwa ni mabadiliko ya tabianchi imesababisha kuwapo na 'tabia mbaya' kiasi cha kufanya maisha hasa katika mataifa yanayoinukia kimaendeleo kuwa ya mihangaiko makubwa kila kukicha.

Ingawa kanuni ya maisha inataka 'kuacha kulaza-damu' bali kuhangaikie maslahi kwa bidii ili kula chakula, kiuhalisia hali ya mazingira imekuwa ngumu kiasi cha binadamu katika mataifa yanayoendelea, kutokwa jasho kiasi cha kupindukia.

Ukame umezidi zaidi hasa kwa miongo miwili iliyopita. Kadhalika, mvua ikinyesha ni hatari kutokana na mafuriko na kusababisha maafa.

Hali imekuwa ngumu hata wanyamapori nao wanahangaika mno kutafuta chakula na maji mpaka kuvamia makazi ya watu na kusababisha taharuki kubwa.



Mwalimu akifundisha wanafunzi kuhusu mazingira. **PICHA: MTANDAO**

Haya yote maana yake nini au yanaashiria kitu gani? Ni matokeo ya uharibifu mkubwa wa mazingira unaofanyika bila kujali athari zake kwa viumbe wengine. Hii ndiyo hali tunayoishuhudia sasa. Kimsingi hayo ni matokeo ya kutoitii sauti na maagizo ya Muumba na kukosa hekima na maarifa katika kuitawala 'dunia na vyote vilivyomo'. Sasa binadamu wanahangaika sana kutokana na kufanya mambo kinyume na mapenzi ya Mungu.

Tujiulize iweje tuangamizwe kwa ugonjwa usioeleweka au maradhi yanayozuka bila kujua chanzo chake? Wakati mwingine kutokana na mahangaiko ya binadamu huwa nasikia watu wakisema "akili nyingi maarifa kidogo".

Kauli hizo zinaashiria kwamba binadamu tunajiletea hali ya 'kuangamizwa' kutokana na athari za mabadiliko ya tabianchi kwa kukosa maarifa ya kutosha au kwa kupuuzia ukweli.

Maendeleo-endelevu tunayahitaji lakini inatakiwa tutumie mbinu za kisayansi na teknolojia zisizohatarishi kwa maisha yetu na kwa kuzingatia maisha ya vizazi vijavyo. Tusiwe na roho za uchoyo na ubinafsi uliokithiri kiasi cha kujilimbikizia mali na fedha nyingi wakati rasilimali hizo zingetumika kwa faida ya wengi bila kuathiri mazingira.

Mojawapo ya mipango-mikakati ni kuingiza "Elimu ya Mazingira" katika mitaala ya shule na vyuo hapa Tanzania ili kuwajengea uwezo vijana waweze kupambana na hali ya hewa isiyotabirika kirahisi lakini pia inayoathiri mihimili ya uhai kutokana na uharibifu mkubwa wa mazingira.

Natambua kuna mikakati inayoendelea kufanikisha suala hili muhimu mfano, elimu ya misitu katika shule za sekondari na vyuo. Hata hivyo vyombo husika ikiwamo Wizara ya Elimu, TAMISEMI, Maliasili na Utalii, Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira, vyuo kama Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA), Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam (UDSM).

Aidha, Chuo Kikuu Huria Taasisi za Elimu, mfano Elimu ya Watu Wazima, taasisi za utafiti mbalimbali kama TAFORI, TAWIRI, TAFIRI, pamoja na kilimo na mifugo na wadau wengine washirikishwe kikamilifu.

### CHA KUFANYA

Elimu ya mazingira katika shule ianzie ngazi ya chini kabisa mfano, shule za awali na za msingi, watoto wazoeshwe picha mbalimbali au mifano halisi kama mimea na miti, misitu, wanyama, ili waanze kuuelewa uhusiano uliopo kati ya misitu, mvua na maji yanayotiririka kutoka katika maeneo yenye misitu kupitia chemichemi hadi mito.

Kadhalika, katika shule za msingi wanafunzi wazoezwe kuyatambua mazao mbalimbali na uhusiano wake katika matumizi bora ya ardhi, misitu na wanyamapori.

Katika shule za sekondari na vyuo mitaala iwawezeshe kujua namna ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa kuwapa maarifa zaidi kuhusu hatua za kuchukua ili kupambana na changamoto zitokanazo na 'mabadiliko husika'.

Elimu na maarifa watakavyovipata vizingatie uwezo wao kusaidia uongozi vijijini kuhifadhi ardhi na maliasili zilizoko pia namna ya kuzitumia kwa misingi endelevu ikiwa ni pamoja na kupitisha na kusimamia matumizi bora ya ardhi.

Wakulima na wafugaji wazingatie kilimo na ufugaji kijani, misitu ya asili itunzwe na kutumiwa kwa misingi endelevu. Wataalamu wa misitu, ufugaji nyuki, kilimo na afya wapunguze muda wa kukaa ofisini ili watumie zaidi wakiwaelimisha na kuwasaidia wakulima na wafugaji namna bora ya kukabiliana na mabadiliko hayo.

Wanafunzi waanze kufahamu na kuelewa vizuri nini maana ya vyanzo vya maji kama, misitu lindi maji, mito, mabwawa, maziwa na ukanda wa bahari. Wakifahamu tangu ujana jinsi ya kuvitunza na kuviendeleza tutapiga hatua kubwa katika kutunza mazingira.

Katika maeneo ya shule na vyuo kuwepo sehemu ambazo wanafunzi wanaweza kufanya mazoezi ya namna ya kuhifadhi udongo kupitia shughuli za kilimo au ufugaji pamoja na kupanda miti ya matunda ya mbao na nguzo.

## Mabegi makubwa, mazito kwa mwanafunzi ni kumwandaa...

**INATOKA UK.11**

Na kukagua mabegi ya watoto wao ili kuona nini wamebeba na kama kinatakiwa kubebwa kwa muda au siku hiyo.

Pia kuwasaidia watoto wao kwa kufuatilia ratiba za masomo ili waweze kuchukua daftari zitazotumika kwa siku hiyo pekee.

Daftari nyingine zisizotumika kwa siku ziachwe nyumbani mpaka siku ya somo itakapofika na kuhitajika, pengine, utaratibu huu unaweza kuwa mgeni na mgumu kwa watoto kuufuata kutokana na mazoea ya hapo awali ila ufuatiliaji wa wazazi na walezi ukiendelea kwa muda mrefu basi wanafunzi watauzoea na kuutekeleza bila shida.

Watoto hawa wanatakiwa kujifunza mambo mema ya kubeba daftari na vitabu vichache hasa vile vinavyohitajika kwa siku ili kuepuka kubeba kila kitu na wakati mwingine vitabu huchanika na kuharibika.

Hivyo kuwa na mabegi makubwa na mazito kila siku waendapo shuleni ambayo huathiri afya zao sasa au hapo baadaye si jambo jema.

### ANGALIZO MUHIMU

Wito wangu kwa jamii ni kuwa ianze sasa kuwasaidia watoto wanaokwenda shuleni kuachana na mizigo kila siku kulinda afya zao.

Hii itasaidia sana kuwalinda watoto na wanafunzi dhidi ya matatizo ya kiafya yanayoweza kuwapata mfano, upumuaji, kuumwa mgongo na tatizo la kusagika kwa pingili za uti wa mgongo, maumivu ya mabega, shingo, kiuno na miguu na matatizo mengine mengi.

Na mwisho watoto hawa hushindwa kufanya vizuri katika masomo yao kwa kuwa inakuwa vigumu kuwa na utulivu na kusikiliza walimu. Kwa mfano, kama ratiba ya masomo inaonyesha kutakuwa na vipindi vinne kwa siku basi mtoto achukue daftari za masomo manne na sio zote 12 na vitabu ambayo havitumika kwa siku husika.

Jamii nzima kuanzia walimu, wazazi na walezi, wanasiasa Wizara ya Elimu na ya Afya zijitahidi kuwaelekeza na kuwasaidia watoto ili kuachana na mazoea hayo.

Tukumbuke watoto ambao ni wanafunzi wa leo ni taifa la kesho hivyo lazima tujitahidi kuwaandaa na pia kuwalinda kiafya ili waweze kuja kutoa mchango wao katika ujenzi wa taifa muda wao ukifika.

**Mwandishi ni mhadhiri msaidizi katika fani ya Usimamizi, Ufuatiliaji na Tathmini Miradi ya Afya, MUHAS. MAONI: 0757-645746**





## Wabunge watakiwa kuwa vinara matumizi ya dijitali

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

WABUNGE wametakiwa kuwa vinara wa matumizi ya kidijitali ili kusaidia kutunga sheria zenye matumizi sahihi ya kimitandao.

Aidha wameombwa kusaidia kupeleka elimu ya matumizi ya kidijitali kwa mikoa ya pembezoni pamoja na maeneo ya vijijini.

Mbunge wa Viti Maalum na Mkurugenzi wa Shirika la Omuka Hub, Neema Lugakingira, alisema hayo wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya masuala ya kidijitali kwa wabunge yaliyofanyika mwisho wa wiki jijini hapo.

Mafunzo hayo yalitolewa na shirika hilo kwa kushirikiana na Shirika la Small Media la London la nchini Uingereza.

Lugakingira alisema wabunge wanatakiwa kuwa vinara katika matumizi ya kidijitali ili kusaidia jamii wakati wa kutunga sheria mbalimbali za kimitandao.

"Mimi ni mbunge kupitia asasi za kiraia na mwanzilishi wa Shirika la Omuka Hub lenye makao makuu yake Mkoa wa Kagera lakini kwa kushirikiana na Shirika la Small Media kuwajengea uwezo wabunge wenzangu,"alisema.

Alibainisha kuwa dunia ya sasa inakwenda kidijitali na fursa nyingi na maendeleo yanapatikana kupitia njia hiyo inayounganisha watu wengi.

Kadhalika alisema kutokana na mwenendo huo shirika hilo liliandaa mafunzo hayo ya siku moja kwa ajili ya kuwajengea uwezo wabunge kuhusu masuala ya kidijitali.

Aliongeza kuwa wabunge wanatakiwa kuyajua matumizi sahihi ya mitandao ili kusaidia kutunga sheria za kuwalinda watumiaji wa njia hizo za kidijitali.

Mwakilishi wa Shirika la Small Media kutoka London Uingereza, Catherin Anite, alisema shirika hilo limekuwa na jukumu la kuwajengea wananchi haki ya kupata huduma hizo.

Alisema kuwa kuna baadhi ya nchi duniani wamekuwa wakinyima haki ya kidijitali wananchi hasa nyakati za uchaguzi.

Alisema nchi zote zinatakiwa kuwa na sheria za kuwalinda watumiaji ili kupata za kiuchumi.

Aliongeza kuwa mifumo hiyo imekuwa ikiwasaidia wananchi kufanya biashara kwa kuwasiliana ndani na nje ya nchi husika.

Mwenyekiti wa Bunge, Najma Murtaza Giga, alisema Tanzania imeingia kwenye mikataba mingi ya haki za binadamu, kwamba Katiba ya nchi pia imetoa uhuru wa kila mwananchi kupata haki ya kupata na kutoa habari na sheria za kulinda haki za watumiaji wa mitandao.

Alibainisha kuwa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania( TCRA) wamekabidhiwa jukumu la kusimamia maudhui na matumizi ya mitandao nchini.

Alisema kuna sheria ya kuruhusu matumizi ya huduma hizo lakini kuna sheria inayozuia aina ya matumizi mabaya ya mitandao hivyo wananchi wazingatie.

# Vijana 97,000 wapata elimu ya uanagenzi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

VIJANA 97,000 nchini wamepata mafunzo ya uanagenzi yanayotolewa kupitia programu ya kukuza ujuzi iliyopo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu inayolenga kufungua fursa nyingi za ajira kwa vijana.

Mkurugenzi wa Ajira na Ukuzaji Ujuzi wa ofisi hiyo, Ally Msaki, alisema mafunzo hayo yalianza kutolewa mwaka 2017 kwenye vyuo vya ufundi 92 nchini na yanagharamiwa kwa asilimia 100 na serikali.

Alisema mwaka 2017 Tanzania iliandaa mwongozo wa mafunzo ya uanagenzi ili vijana wapate ujuzi utakaowasaidia kujiajiri na kuajiriwa.

"Mwaka 2022 Tanzania ilishiriki mkutano mkuu wa Shirika la Kazi Duniani (ILO) na kuandaa mwongozo wa mafunzo ya uanagenzi kimataifa.

Hii ilitokana na kuwa nchi ya mfano kwenye uanagenzi na Tanzania ilitakiwa kutoa uzoefu wake wa mafunzo haya ambayo asilimia 60 ya muda wa mafunzo mtu anatakiwa kufanya akiwa eneo la kazi," alisema.

Alibainisha kuwa mafunzo hayo ni ya miezi sita na fani zinazotolewa ni ufundi umeme wa majumbani na viwandani, umeme wa jua, useremala, ufundi magari, umeme wa magari na uchomeleaji na uungaji vyuma.

Zingine ni utengenezaji wa vifaa vya aluminium, upishi, uhudumu wa hoteli na vinywaji, ushonaji, uchenjuaji wa madini, ufundi bomba, ufundi uashi, uwekaji wa terazo na marumaru, ufundi viyoyozi na majokofu.

Alifafanua kuwa kwa mwaka 2022/23 vijana 11,975 wanatarajia kupata mafunzo na hadi kufikia Januari mwaka huu vijana 7,760 wamepatiwa ujuzi, huku wengine 4,215 wakitarajiwa kuanza mafunzo mwanzoni mwa mwezi ujao.

"Kwa mwaka huu wa fedha tayari Sh. bilioni 1.5 zimeshakopwa na vijana waliomaliza mafunzo," alisema.

Hata hivyo alisema ili kuwapatia vijana ujuzi wa kitaalamu zaidi wameamua kufungua vituo atamizi katika mikoa minne ya Dar es Salaam, Lindi, Singida na Kigoma.



Baadhi ya wabunge wakiingia bungeni jana kushiriki kikao cha tano mkutano wa 10 baada ya mapumziko ya mwisho wa wiki. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Kesi Katibu Anglikana, Baraza la Wadhamini Februari 22

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KESI ya aliyekuwa Katibu Mkuu wa Kanisa Aglikana Tanzania, Dk. Mecka Ogunde dhidi ya Baraza la Wadhamini wa kanisa hilo iliyofunguliwa katika Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) Dodoma kuanza kusikilizwa Februari 22, mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari jana baada ya kuahirishwa kwa shauri hilo, Wakili wa mlalamikaji, Godfrey Wasonga, alisema shauri lao la mgogoro wa kikazi baina ya Dk. Ogunde dhidi ya Baraza la Wadhamini wa Kanisa Aglikana Tanzania lilitajwa jana.

"Leo ndiyo ilikuwa siku ya kutajwa kwa shauri letu lakini wenzetu wa upande wa pili walikuwa wanadai kuwa wanataka shauri hili lisimame kusikilizwa ili kupisha maamuzi ya Mahakama ya Rufani. Wakili wa mlalamikiwa, Denis Malamba alisema jana ilikuwa siku ya kutajwa kwa shauri hilo lakini tayari wameshapeleka maombi yao ya kupeleka shauri hilo Mahakama ya Rufani.

"Leo tulikuja kwa ajili ya kutajwa kwa shauri hili na kuangalia kama shauri hili linaweza kusubiri kwanza maamuzi ya Mahakama ya Rufani ndipo kuendelea au vinginevyo kwa kuwa rufani ni haki yetu na wakati wowote ambapo tunaona kuwa ipo haja ya sisi kufanya hivyo tunafanya hivyo," alisema.

Desemba 27, mwaka jana chini ya Jaji Masaju Mahakama Kuu Kanda ya Dodoma ilitupilia mbali maombi ya marejeo yaliyowasilishwa na wadhamini wa Kanisa Aglikana Tanzania kuhusu shauri hilo.

Aidha, Mahakama Kuu Kanda ya Dodoma, ilitupilia mbali maombi ya Baraza la Wadhamini wa Kanisa hilo kupinga Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) Mkoa wa Dodoma kuendelea kusikiliza mgogoro huo wa kikazi nje ya muda.

Akizungumza na waandishi wa habari Julai 27, mwaka jana, wakili wa mlalamikaji Willison Ogunde, alisema wameamua kufunga shauri hilo baada ya Baraza la Wadhamini wa Kanisa Anglikana Tanzania, kushindwa kufika makubaliano na mteja wake.





# H'shauri yakwama kukamilisha ujenzi maboma 14 ya zahanati

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya imeshindwa kukamilisha ujenzi wa maboma 14 ya zahanati yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi kwenye vijiji mbalimbali kutokana na uhaba wa fedha.

Kutokana na hali hiyo, madiwani wa halmashauri hiyo wameiomba serikali kusaidia kukamilisha maboma hayo ili wananchi waanze kupata huduma mapema.

Wakizungumza kwenye kikao cha baraza hilo cha kupitisha Bajeti ya Halmashauri ya Wilaya ya Kyela ya mwaka 2023/2024, madiwani hao walisema walidai kuwa wakitumia mapato ya ndani itachukua muda mrefu kukamilisha.

Diwani wa Viti Maalum, Tumaini Mwakatika, alisema kuwa bajeti iliyotengwa na halmashauri hiyo kwa mwaka wa fedha wa 2023/2024 inaonyesha kuwa maboma mengi yaliyojengwa na wananchi hayawezi kukamilishwa kutokana na uhaba wa fedha.

Alisema kuwa maboma hayo yasipokamilishwa kwa wakati, yatasababisha wananchi kukata tamaa ya kufanya shughuli za maendeleo au nguvu zao kupotea ikiwa majengo hayo yataharibika.

"Wananchi walijitolea kujenga maboma hayo kwa nguvu zao wenyewe wakiamini kuwa wakimaliza kuyajenga serikali itayapaua na kuyafanyia umaliziaji kama ambavyo sera ya serikali inavyosema ili yaanze kutoa huduma, ikiwa serikali itayaacha basi wananchi watakata tamaa na pengine nguvu zao zitakuwa zimepotea," alisema Tumaini.

Aliiomba serikali kupitia Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa (TAMISEMI) kuangalia uwezekano wa kutoa fungu maalum la fedha ili kukamilisha maboma hayo.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, Katule Kingamkono, alisema kuwa halmashauri hiyo inayo maboma 14 ya zahanati ambayo ujenzi wake umekamilika kwa kutumia nguvu za wananchi na sasa yanasubiri serikali iyakamilishe.

Alisema kuwa zaidi ya shilingi bilioni moja zinahitajika ili kukamilisha ujenzi wa maboma hayo, lakini halmashauri yake haina uwezo wa kupata kiwango hicho cha fedha katika kipindi cha mwaka mmoja wa bajeti.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, Kenneth Izirano, alisema kuwa katika bajeti ya mwaka wa fedha wa 2023/2024, ambayo ilipitishwa juzi na Baraza la Madiwani la Halmashauri hiyo, zimetengwa fedha kwa ajili ya kukamilisha maboma sita kati ya 14 yaliyoko.

Alisema ombi la madiwani la kuitaka serikali kusaidia ukamilishwaji wa maboma hayo lina mashiko kwa kuwa ni kweli halmashauri hiyo haina uwezo wa kuyakamilisha kwa kutumia fedha za ndani katika kipindi cha mwaka mmoja.

Alisema ili maboma hayo yote yakamilike yanahitaji kutengewa fedha kwenye bajeti za miaka mitatu mfululizo, jambo ambalo litasababisha maboma mengi yakae muda mrefu bila kukamilika.

"Wakati sisi kama halmashauri tukiendelea kutenga fedha za kukamilisha maboma ya zahanati yaliyoko, wananchi katika vijiji vingine nao wanaendelea kujenga maboma mengine, hivyo kama tutategemea vyanzo vyetu vya ndani itatuchukua muda mrefu kuyamaliza, ndiyo maana madiwani wameona waiombe serikali kuu iingilie kati," alisema Izrano.

Kwa mujibu wa sera ya ujenzi wa zahanati ni kwamba wananchi wanatakiwa kujenga maboma na kisha halmashauri kukamilisha ili wananchi waanze kupata huduma.

## Maambukizi VVU Tunduma yaongezeka

**Na Nebart Msokwa,** TUNDUMA

HALMASHAURI ya Mji wa Tunduma mkoani Songwe imesema takwimu za maambukizi ya Virusi vya Ukimwi katika mji huo zimeongezeka kutokana na kukithiri kwa biashara ya ngono na mwingiliano wa shughuli za kiuchumi baina ya Tanzania nchi jirani.

Takwimu za mwaka 2016/2017 zinaonyesha Mkoa wa Songwe maambukizi kuwa juu kuliko takwimu za kitaifa kwa kuwa na asilimia 5.8 huku takwimu za kitaifa za maambukizi yakiwa asilimia 4.7.

Mratibu wa Tume ya Kudhibiti Ukimwi Mkoa wa Songwe, (TACAIDS), Emmanuel Petro, aliyasema hayo baada ya Shirika la HJFMRI kuzindua mradi wa Dreams utakaolenga kuwawezesha vijana na mabinti kutambua hali zao na kuanzisha miradi ya kiuchumi.

Petro alisema hali ya maambukizi inakuwa siku hadi siku kutokana na jamii kutokubali kubadilika na kutumia eneo la mpakani kama sehemu ya kitega uchumi kwa 'madada poa' kutoka mikoa mbalimbali nchini.

"Mwingiliano wa shughuli za kiuchumi baina ya nchi mbili ya Tanzania na Zambia ndio unachochea kasi ya watu kutoka mikoa mbalimbali kuja kutafuta fedha au kwa kufanya ngono zisizo salama na hivyo kuchochea ongezeko la maambukizi mapya ya UKIMWI," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la HJFMRI, Dk. David Maganga, alisema wamelazimika kuleta mradi huo kutokana na hali ilivyo na kwamba watu watano kati ya 100 wanapata maambukizi mapya ya UKIMWI kwa siku.




Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Saad Mtambule (kushoto) na Mkuu wa Shule ya Msingi Minazini, Mariam Adam (kulia), wakipokea msaada wa madawati kutoka kwa Rais wa Klabu ya Rotary ya Dar es Salaam, Nikki Aggarwal (katikati), katika hafla ya kukabidhi msaada wa madawati 200 kwa shule hiyo hivi karibuni. Klabu ya Rotary tayari imeshatoa madawati zaidi ya 2,000 kwa shule mbalimbali yenye thamani ya Sh. milioni 300. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TAHLISO yaipa kongole serikali bima ya afya kwa wote

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SHIRIKISHO la Vyuo Vikuu nchini (TAHLISO), limeipongeza serikali kwa kuanzisha mchakato wa bima ya afya kwa wote kwa maelezo kuwa utaratibu huo utasaidia kupunguza tatizo la watu kukosa matibabu kutokana na hali ngumu ya kiuchumi.

Walitoa pongezi hizo jijini Mbeya mwishoni mwa wiki wakati wa mkutano mkuu wa seneti ambao unawashirikisha marais na viongozi mbalimbali wa vyuo hivyo uliofanyika kwa siku mbili.

Viongozi hao walisema bima ya afya kwa wote itasaidia wananchi wa madaraja yote kupata huduma za matibabu bila kuwa na vikwazo na hivyo kusaidia kupunguza vifo.

Rais wa Chuo cha Elimu ya Biashara Dodoma, Hoseni Abdallah, alisema Watanzania wamekuwa wakitumia gharama kubwa kwenye matibabu hasa wanapougua kwa muda mrefu.

Alisema magonjwa huwa hayapigi hodi na hivyo kusababisha baadhi ya watu kupoteza maisha kwa sababu ya kukosa fedha kwa ajili ya matibabu.

Alisema utaratibu huo ulioanzishwa na serikali wa bima ya afya kwa wote ukifanikiwa utawasaidia Watanzania kupunguza gharama za matibabu na hivyo kuwa na uhakika wa matibabu.

Kamishna wa Afya na Mazingira wa Shirikisho hilo, Yolanda Kitama, alisema bima ya afya kwa wote itawasaidia Watanzania kupata matibabu bila kubaguana kulingana na kipato cha mtu ama namna nyingine yoyote.

Alisema viongozi wa shirikisho hilo watashirikiana na serikali kuhamasisha Watanzania na kuhakikisha utaratibu huo unafanikiwa kwa manufaa ya taifa.

Alisema Tanzania haitakuwa nchi ya kwanza kutekeleza utaratibu huo kwa maelezo kuwa baadhi ya mataifa yalishafanya hivyo ikiwamo Rwanda na ikafanikiwa.

Mwakilishi wa Wizara ya Afya, Jackline Tarimo, alisema Tanzania kuna mwamko mdogo wa wananchi kujiunga na bima ya afya na hivyo inahitajika hamasa kubwa ili wajiunge zaidi.

Alisema mpaka sasa ni asilimia 15 pekee ya Watanzania wenye bima za afya, hivyo kusababisha asilimia 85 kuwa katika hatari ya kukosa matibabu ya uhakika endapo watougua.

Alisema watu ambao hawana bima ya afya huwa wanatumia fedha nyingi kwenye matibabu kuliko wale wanaotumia bima hizo akisisitiza kuwa hali hiyo inatokana na wenye bima kuchangiana.

Alisema Watanzania ambao hawana bima ya afya wako hatarini kuwa masikini kutokana na kutumia gharama kubwa kwenye matibabu na wengine huwa wanalazimika kuuza mali ili wapate fedha za matibabu.





Mlezi wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Kaskazini Unguja, Dk. Tulia Ackson, akimkabidhi mwanaushirika wa kikundi cha Yajayo Yanapendeza hati ya boti ya uvuvi wakati akiwa katika ziara ya mkoa huo, Mahonda kwenye ofisi za CCM. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Baadhi ya wafanyabiashara wakaidi kulipa kodi kwa EFD

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Mkoa wa Kusini Pemba, Matar Zahor Massoud, amesema pamoja na juhudi zinazofanywa na Serikali ya Zanzibar ya uhamasishaji wa ulipaji kodi kwa kutumia mashine maalumu za kutolea risiti za elektroniki, lakini kuna baadhi ya wafanyabiashara hawapo tayari kuendana na mfumo huo.

Alisema ni wajibu wa kisheria kwa kila mfanyabiashara kuwa na mashine ya kutolea risiti za elektroniki na kuitumia ili serikali kupata mapato yake inayostahili na kwa ukamilifu wake.

Matar aliyaeleza hayo jana katika ukumbi wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) Gombani Pemba wakati akizungumza na wafanyabiashara wa Mkoa wa Kusini kisiwani humo ikiwa ni mwendelezo wa mikutano yake ya kusikiliza kero kupitia makundi tofauti.

Alisema kuwa kila mmoja anawajibu wa kutambuwa kuwa hakuna serikali yoyote inayokwenda bila ya kuwa na kodi na ndiyo inayoiwezesha kupanga mipango ya maendeleo ya sekta mbalimbali kwa wananchi wake.

Aidha, alisema kuwa serikali ya mkoa huo haitomwonea haya na wala haitomvumilia mfanyabiashara yoyote ambaye hatokwenda kwa majibu wa sheria za nchi wakati akifanya shughuli zake za biashara na nchi inakwenda kwa mujibu wa sheria.

Alisema kumekuwa na visingizio vingi kutoka kwa wafanyabiashara ambayo wanadai kupandisha bei ya bidhaa hiyo jambo ambalo vyingine havina ukweli.

Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato (ZRA) Zanzibar, Yusuph Juma Mwenda, alisema Zanzibar ndiyo nchi pekee kwa nchi za Afrika Mashariki ambayo inatoza kodi ndogo kwa wafanyabiashara wake na imewafanya wafanyabiashara wakubwa wanaoingiza bidhaa Zanzibar kutolipa ushuru wa VAT wala Stamp.

Alieleza kuwa serikali ikitoa mchango wa kupunguza ushuru ili wananchi kufaidika na mahitaji yao mbalimbali ya chakula kutokana na hali zao kimaisha na pale kunapokuwa na matatizo milango ya ofisi zao iko wazi wafanyabiashara waende kuzieleza.

Alisema ZRA siyo maadui kwa wafanyabiashara na wala isijengeke dhana hiyo isipokuwa kila anayestahiki kulipa kodi alipe hata kama ni kidogo.

Mkurugenzi wa Tume ya Ushindani wa Biashara Zanzibar, Moh'd Sijaamini Moh'd, aliwataka wafanyabiashara kuwa wakweli na kuteremsha bei ya bidhaa na kutoa taharuki kwa wananchi.

Alisema kuwa taasisi yake itapita kwenye maduka kuangalia hali ya bei iliyoko lakini serikali haitomwonea huruma wala haitomwonea mfanyabiashara anayeuza mchele kwa kilo Sh.3,000 na badala yake kuuza kwa Sh. 1,700 kwa kilo.

# Wavuvi watakiwa kuwachagua viongozi watakaotatua kero zao

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAVUVI katika Kisiwa cha Unguja wametakiwa kuchagua viongozi sahihi watakaosimamia kamati ya uvuvi za mkoa.

Pia wametakiwa kuchagua viongozi ambao watatatua matatizo yao ili waendelee na uvuvi endelevu wenye tija kwa taifa.

Rai hiyo ilitolewa na Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Uvuvi na Mazao ya Baharini Zanzibar, Dk. Salum Suod Hammed, wakati wa uchaguzi wa kuwachagua wenyeviti wa mikoa mitatu ya Unguja.

Dk. Salum alisema lengo la serikali kuunda kamati ya uvuvi ya mkoa ni kuweka usimamizi wa pamoja baina ya serikali na wananchi husika katika ngazi ya mkoa.

Alisema kuwapo kwa kamati ya mkoa kutasaidia kuwaunganisha, kuwawakilisha wavuvi ili kuwa na sauti moja juu ya matumizi na usimamizi wa uvuvi unaokubalika kisheria nchini.

Ofisa Uvuvi wa Wilaya ya Kusini Unguja, Omar Mpango, aliwataka wenyeviti wa mikoa waliochaguliwa katika uchaguzi huo kuwa na ushirikiano na taasisi za serikali katika kusimamia rasilimali za bahari ili kuwa na uvuvi endelevu katika maeneo ya bahari.

Wenyeviti wa mikoa wameitaka Idara ya Maendeleo ya Uvuvi na mazao ya baharini kuwafanyia vikao vya mara kwa mara ili kutatua matatizo yanayowakabili wavuvi.

Ameri Talib ni miongoni wa wenyeviti hao aliiomba taasisi husika kuwapatia majukumu yao kwa haraka ili kufanyakazi zao kwa ufanisi zaidi.

# Waziri akemea tabia kinamama kutupa watoto

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Riziki Pembe Juma, amekemea kitendo cha baadhi ya wazazi kuwatupa watoto.

Aliyasema hayo jana wakati alipomtembelea mtoto wa siku mbili aliyetupwa juzi katika maeneo ya Fuoni nje ya Mji wa Zanzibar ambapo mtoto huyo anaendelea kupata matibabu katika Hospitali ya Mnazi Mmoja. Alisema kitendo hicho siyo cha kibinadamu na haipendezi mwanamke kuwa katili kwa kutupa mtoto ambacho alikuwa nacho tumboni kwa muda wa miezi tisa wakati wa ujauzito wake.

"Haipendezi kuona mwanamke anakuwa katili na mwanamke kama huyo anaweza kumdhuru mtu yoyote," alisema.

Hivyo, aliwataka wanawake na wazazi kukomesha vitendo hivyo vya kutupa watoto na kulitaka Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi ili kumjua mama wa mtoto huyo aliyefanya ukatili huo na sheria kuchukua mkondo wake.

Alisema serikali itamlea mtoto huyo kama taratibu na sheria zinavyoelekeza katika kupata haki zake stahiki na kuomba mtoto huyo kupewa jina la Riziki.

Aidha, aliwataka madaktari kutochoka kutoa huduma bora kwa wagonjwa wanaofika hospitalini hapo na kuwapongeza kwa kazi ya kuokoa maisha ya mtoto huyo.

Zubeda Mohammed Hussein kutoka kitengo cha watoto hospitalini hapo alisema kuwa afya ya mtoto huyo inaendelea vizuri.

Aliwataka wazazi ambao hawahitaji watoto ni bora kutumia uzazi wa mpango kuliko kuwatupa watoto ambao hawana hatia yoyote.



Abiria wa mabasi ya mwendokasi wakisubiri kupanda mabasi hayo kwenye kituo cha daladala Mbezi Mwisho Manispaa ya Ubungo Dar es Salaam jana. Wakati mwingine yanachelewa kufika kituoni hapo kutokana na foleni za magari barabarani na kusababisha usumbufu kwa abiria. **PICHA: SABATO KASIKA**

## Wabunge walia ukusanyaji mapato, ahadi 'ambulance'

**Na Romana Mallya**

BAADHI ya wabunge wamehoji kuhusu mfumo wa ukusanyaji mapato na yaliko magari ya kubeba wagonjwa (ambulance) yaliyotakiwa kununuliwa kutokana na fedha za UVIKO-19.

Walihoji hayo jana bungeni jijini hapa kwa nyakati tofauti wakati wanachangia taarifa ya mwaka ya shughuli za Kamati ya Bunge ya Bajeti.

Akizungumzia mwenendo wa ukusanyaji wa mapato, Mbunge wa Viti Maalum, Esther Matiko alisema kama wataweza kuudhibiti, nchi itakusanya zaidi ya Sh. trilioni 40 na kuifanya isiwe tegemezi kwa washirika wa maendeleo.

Alisema taarifa zilizoainishwa kwenye kamati zinazosababisha upotevu wa mapato ni pamoja na mashine za EFD ambapo utafiti wa kina uliofanyika unaonyesha wafanyabiashara hawazitumii.

"Pamoja na kwamba walipakodi ni wachache, wapo milioni nne lakini kati yao wanaolipa ni milioni mbili tu na kufikia Sh. trilioni 24 au 25, tukiziba mianya yote hata hiyo trilioni 40 ni chache sana," alisema.

Alitaja jambo lingine linalopoteza mapato, akijerea taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) 2020/21, kuwa kuna malimbikizo ya madeni ya kodi ambayo hayakusanywi.

"2019/20 madeni ambayo yalikuwa hayakusanywi ni Sh. trilioni 3.86, mwaka 2020/21 yakaongezeka kwa asilimia 96 na kufikia trilioni 7.54, yangekusanywa yangeongezeka sehemu kubwa sana," alisema.

Mjumbe wa Kamati ya Bajeti na Mbunge wa Kibamba, Issa Mtemvu, akichangia kuhusu mikopo, alisema mkopo wa ECF kutoka IMF wa dola bilioni 1.046 sawa na Sh. trilioni 2.4 umetiliwa shaka na kamati kama malengo yanafikiwa.

"Lengo kubwa kwenye mkopo huu wa Sh. trilioni 2.4 ambao ni dirisha la pili, tulichukua kwa lengo kubwa likiwa ni kupunguza uagizaji urari wa nchi badala ya kuagiza tukazalisha.

"Kinachotokea ni changamoto kubwa, ukiangalia ufanisi wa mkopo huu mpaka sasa, ulitolewa mwezi Agosti na masharti yake utatolewa kwa awamu saba kwa vipindi vya miezi 40, lakini mpaka sasa maeneo yote ya kipaumbele kilimo, uvuvi, nishati maji, nishati ya umeme hakuna hata moja iliyofika asilimia 30," alihadharisha.

# Bunge latoa angalizo mfumo wa utoaji leseni za udereva

**Na Romana Mallya,** DODOMA

BUNGE limesema mfumo wa sasa unaotumika kutoa leseni za udereva unatoa mwanya kwa baadhi ya madereva ambao hawana sifa wala vigezo, kuzipata na hivyo kuchangia ajali za barabarani.

Kutokana na hali hiyo, Bunge limeazimia serikali ianze mchakato wa kuutazama upya mfumo huo ili kuwa na ulio imara ambao utatoa fursa kwa madereva waliokidhi vigezo pekee kupata leseni.

Hayo yamo kwenye taarifa ya mwaka ya shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama iliyosomwa jana bungeni jijini hapa na Mwenyekiti wake, Vita Kawawa.

Mwenyekiti huyo alisema kwa kipindi cha mwezi Oktoba hadi Desemba 2022, matukio ya ajali yaliyosababisha vifo ni 281 kulinganishwa na matukio 273 yaliyoripotiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2021.

"Hili ni ongezeko la makosa manane sawa na asilimia 2.9. Kwa kipindi hicho, idadi ya watu waliopoteza maisha kutokana na ajali ni 382 kulinganishwa na idadi ya watu 367 waliopoteza maisha kwa kipindi kama hicho mwaka 2021. Hili ni ongezeko la watu 15 sawa na asilimia 4.1," alisema.

Kawawa alisema uchambuzi wa kamati unaonyesha ajali zimekuwa zikichangiwa na baadhi ya askari barabarani kujihusisha na rushwa na hivyo kushindwa kutimiza wajibu wao katika kushughulikia makosa ya barabarani.

Pia alisema uhaba wa vitendea kazi kama vile magari ya doria kwenye barabara kuu, taa za kuongozea magari, upungufu wa tochi za kupima mwendo, upungufu wa kamera na vipima ulevi.

"Kukosekana kwa utashi wa kisiasa kwa baadhi ya wanasiasa na hivyo utekelezaji wa sheria za usalama barabarani. Mathalani, kuzuia askari kuwakamata bodaboda au madereva bajaji waliofanya uvunjifu wa sheria.

"Ubovu wa baadhi ya barabara wakati mwingine husababisha ajali, hulka za kibinadamu kuamini kuwa ajali hazizuiliki na hivyo kuendesha pasipo kuzingatia sheria, kuwa na madereva wengi wasio na sifa ya udereva unaochangiwa na hali ya mfumo kutoa leseni kwa watu wasio na sifa," alibainisha.

Pia alisema kamati imebaini kuwa katika siku za karibuni kumeibuka wimbi la magari ya watu binafsi, taasisi binafsi na ya umma, kufungwa ving'ora kinyume cha utaratibu ilhali wakiwa hawana uelewa kuhusu matumizi yake.

Alisema hali hiyo inahatarisha usalama kwa watumiaji wengine wa barabara.

Alisema Bunge linaazimia serikali kudhibiti matumizi holela ya ving'ora kwenye magari na kuhakikisha vinafungwa kwenye magari yanayostahili.

Pia Bunge limeazimia serikali iendelee kudhibiti uendeshaji mbovu wa madereva bodaboda kwa kusimamia ipasavyo Sheria ya Usalama Barabarani kwa kuwa uendeshaji wao umekuwa moja ya vyanzo vya ajali.

**KUPOTEA KWA CHETI**



**JULIANA MUSHI,** anatangaza kupotelewa cheti cha kidato cha nne chenye Index namba **S0320/0066** cha mwaka **1990** katika shule ya sekondari ya **LAKE**, kilichotolewa na Baraza la Mitihani, yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi **RB:MWA/NYA/RB44549/2023** ama simu namba **0769444462**

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOROGORO**
**SHERIA YA UMILIKISHAJI**
**WA ARDHI YA MWAKA 1999**
**KUPOTEA KWA BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI**
**BARUA YA TOLEO YENYE KUMB. NA. MMC/LD/12509**
**MMILIKI ALIOANDIKISHWA: JUMA MAULIDI WA S.L.P 853, MOROGORO.**
**ARDHI: KIWANJA NA. 103 KITALU "BB" MOROGORO MJINI-MANISPAA YA MOROGORO**
**MUOMBAJI: JUMA MAULIDI S.L.P 853, MOROGORO.**

Taarifa inatolewa kwamba **BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI** iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa **NAKALA HALISI YA BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI** iwapo hakuna pingamizi litakalo tolewa kwa muda wa mwezi mmoja toka tarehe ya taarifa hii itakapotangazwa katika gazeti.

**HATI YA BARUA HALISI YA TOLEO** ikionekana , irudishwe kwa **MKURUGENZI WA MANISPAA – MOROGORO S.L.P 166 MOROGORO.**

AMBARA H.P
KNY: MKURUGENZI WA MANISPAA
MOROGORO

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**RASHID IDDY RASHID**

anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 209 ARV – TOYOTA CORSA.** Chassis namba **EL510026205.** Engine namba **4E1330848.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/URA/RB/433214/2022**

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI.**

**ROSEE MAKENGE PHARMACY LIMITED**

inatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOYA SUCCED** yenye usajili namba **T469DPD.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chchote cha polisi.

POLISI TAARIFA:
**SIM/MAS/RB/39769/2023.**

# TEF yawatoa hofu wadau mchakato kuifumua Sheria ya Habari 2016

**Na Mwandishi Wetu**

JUKWAA la Wahariri Tanzania (TEF) limewataka wadau wa habari nchini kuwa na subira kwa kuwa Muswada wa Mabadiliko ya Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari ya 2016, utawasilishwa bungeni wakati wowote kabla mkutano wa 10 wa Bunge unaoendelea jijini Daodoma, haujaahirishwa mwishoni mwa wiki hii.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Mwenyekiti wa TEF, Deodatus Balile alipozungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam.

Balile alikuwa akitolea ufafanuzi kuhusu baadhi ya maswali aliyokuwa akiulizwa na wadau wa habari nchini walihoji hatima ya muswada huo kwa kuwa ratiba ya vikao vya Bunge haionyeshi ni lini muswada huo utawasilishwa bungeni kama serikali ilivyoahidi.

Kwa mujibu wa Balile, muswada huo haukuwekwa kwenye ratiba ya vikao vya Bunge moja kwa moja kama ilivyozoeleka kwa kuwa utawasilishwa bungeni kupitia marekebisho madogo ya sheria mbalimbali.

"Muswada wa Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari utaingia bungeni kwenye vikao vya mkutano wa Bunge vinavyoendelea hivi sasa jijini Dodoma.

"Nimeona watu wengi walioangalia ratiba ya Bunge wananipigia simu, wanasema 'sasa mbona huo muswada haumo kwenye mawasilisho ya sheria zitakazowasilishwa?' Wadau wanasema wameona tarehe 9 na 10 kuna Muswada wa Bima ya Afya, lakini hawaoni sheria ya masuala ya kihabari.

"Lakini, hakika mimi ninazo taarifa za uhakika, kwamba tusiwe na wasiwasi, muswada utaingizwa bungeni isipokuwa kitakachobadilika nadhani hatutatoa muswada huo kwa njia ya kawaida kama utakavyokuwa Muswada wa Bima ya Afya.

"Kitakachotokea ni kwamba muswada huo utaingizwa katika utaratibu wa marekebisho madogo ya sheria mbalimbali.

"Kwa hiyo, tuendelee kusubiria huku tukiendelea kuwasiliana na mamlaka husika, tukiwasiliana na serikali pamoja na watunga sera ili kuona ni kwa namna gani huo muswada utawasilishwa bungeni," alisema Balile katika ufafanuzi huo.

Kwa kipindi kirefu sasa, wadau wa habari nchini wamekuwa wakilalamikia Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari ya Mwaka 2016 kwa kile wanachodai ina baadhi ya vifungu vinavyokandamiza uhuru wa habari nchini.

Kutokana na hali hiyo, wadau hao wamekuwa wakishauri serikali ifanyie marekebisho sheria hiyo kwa kuondoa vifungu vinavyolalamikiwa ili Tanzania iwe ni moja ya nchi zinazothamini taaluma ya habari duniani.

Wakati mijadala hiyo ikiendelea katika majukwaa mbalimbali, mwishoni mwa mwaka jana, Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, alisema jijini Dar es Salaam kwamba serikali inathamini taaluma ya habari kwa kuwa inajua umuhimu wa taaluma hiyo.

Katika kuthibitisha kauli yake, alisema serikali itawasilisha bungeni muswada wa marekebisho ya sheria hiyo wakati wa Bunge la Januari mwaka huu ili Bunge lijadili sheria hiyo na kuiboresha kwa kadri itakavyowezekana.

# DC apiga marufuku kamari kwa wanafunzi

**Na Elisante John,** SINGIDA

MKUU wa Wilaya ya Singida, Paskasi Muragili, amepiga marufuku watoto na wanafunzi kuingia kwenye maeneo inakochezeshwa michezo ya kamari ili kuwaokoa na hatari ya kulawitiwa na vijana wenye ushawishi wa kifedha.

Muragili alitangaza zuio hilo mwishoni mwa wiki alipozungumza na madiwani kupitia mkutano maalum wa bajeti wa Baraza la Madiwani Manispaa ya Singida.

Alisema sambamba na marufuku hiyo, wanaosimamia na kuendesha michezo hiyo wahakikishe wana leseni halali kutoka Manispaa ya Singida ili wajulikane mahali walipo kwa ajili ya kurahisisha upatikanaji wao.

"Kuanzia leo ni marufuku kwa watoto na wanafunzi kuingia na kucheza 'play station'... Ofisa biashara upo! Hakikisha kuanzia sasa wote wanaoendesha michezo hii, wanakata leseni," aliagiza.

Wakichangia mjadala huo, baadhi ya madiwani wakiwamo, Margreth Malecela, Saidati Mzirai na Geofrey Mdama, waliitaka jamii kushirikiana na viongozi kutokomeza vitendo vya ulawiti vinavyoenea kwa kasi nchini.

Walisema wazazi, walezi na jamii kwa ujumla wasipotoa ushirikiano wa kutosha kwa viongozi na serikali kwa ujumla, tatizo hilo litaendelea kuwapo na hivyo kuwaathiri watoto, vijana na hata kizazi cha sasa na kijacho.

Margreth Malecela alitoa angalizo kwa jamii kuwalinda watoto bila ya kuwabagua, akitaka serikali iwachukulie hatua kali za kisheria, watakaojihusisha na ulawiti dhidi ya watoto.

Katika mkutano huo wa baraza, yalipitishwa makadirio ya bajeti ya zaidi ya Sh. bilioni 33.4 kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kulinganishwa na Sh. bilioni 37.8 za bajeti ya mwaka huu.



Ofisa Uhusiano wa Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML), Dorine Denis (kulia), akikata utepe kuashiria uzinduzi wa madarasa mawili yaliyojengwa na kampuni hiyo kwenye Shule ya Msingi Kiziba iliyoko Kijiji cha Mwenegeza wilayani Geita. Dorine alimwakilisha Mkurugenzi Mkuu wa GGML, Terry Strong. Kushoto ni Ofisa Mtendaji wa Kata ya Nyakagomba, Christopha Amos. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# GGML yakabidhi madarasa Shule ya Msingi Kiziba

**Na Mwandishi Wetu,** GEITA

KATIKA kuunga mkono juhudi za serikali za kuboresha elimu na kulea kizazi kijacho ambacho kitasaidia taifa kufikia malengo ya kiuchumi na kimaendeleo, Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML) imejenga na kukabidhi vyumba viwili vya madarasa kwa Shule ya Msingi Kiziba iliyoko Kijiji cha Mwenegeza, Kata ya Nyakagomba wilayani Geita mkoani Geita.

Madarasa hayo mawili yenye thamani ya Sh. milioni 42, yanalenga kusaidia kutoa mazingira mazuri ya kujifunzia kwa wanafunzi ambao ufaulu wao umeathiriwa na mazingira magumu ya kujifunzia.

Akizungumza katika hafla ya kukabidhi madarasa hayo mwishoni mwa wiki mjini Geita kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa GGML, Terry Strong, Ofisa Uhusiano wa kampuni hiyo, Dorine Denis, alisema elimu ni nguzo muhimu ya jamii, hivyo bila elimu ni vigumu kupata maendeleo.

Alisema elimu inaweza kubadilisha maisha ya watu na ni mwelekeo wa miradi yao ya uwekezaji wa jamii.

"GGML inaamini kuwa wananchi wa Tanzania ndio mtaji mkubwa wa kampuni hii na siku zote imekuwa ikiunga mkono juhudi za serikali za kuboresha elimu na kujenga kizazi kijacho ambacho kitasaidia Taifa la Tanzania kufikia malengo yake makubwa ya kiuchumi na kimaendeleo.

"GGML imedhamiria kuchochea maendeleo endelevu ya jamii zinazozunguka mgodi na imedhihirisha hilo mara kwa mara kwa kushirikiana kikamilifu na serikali katika kuboresha huduma za jamii ikiwamo elimu, afya, maji na barabara pamoja na shughuli nyingine za kiuchumi kwa jamii zinazozunguka mgodi huo.

"Tunakusudia kuwa na urithi uliojengwa na uchumi endelevu wa ndani unaoweza kukaa muda mrefu, hata baada ya shughuli za uchimbaji madini mkoani Geita kumalizika," alisema.

Aliongeza kuwa GGML inafanya kazi ya kuunga mkono malengo ya Serikali ya Tanzania ya ukuaji thabiti wa uchumi na maboresho ya miundombinu ya kijamii.

"Hii inaendana na thamani yetu ya msingi ya kusaidia serikali katika kukuza ukuaji wa uchumi wa muda mrefu kwenye jamii tunakofanyia kazi.

"Kwa hiyo, nimefurahishwa kwamba ujenzi wa madarasa haya umetokana na juhudi za ushirikiano kati ya serikali, jamii mwenyeji na GGML," alisema.

Vilevile, aliahidi kuwa GGML itaendelea kushirikiana na Serikali ya Tanzania na wadau wengine ili kufikia lengo la sekta ya madini la kuchangia asilimia 10 kwa Pato la Taifa ifikapo mwaka 2025.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Kiziba, Beatus Mwandu, aliishukuru GGML kwa ujenzi wa madarasa hayo, ikizingatiwa shule hiyo bado inakabiliwa na uhaba wa madarasa huku mengine yakiwa yamechakaa.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Nyakagomba, Christopha Amos, aliishukuru GGML kwa msaada huo na kuahidi kufikisha kilio cha changamoto nyingine kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Geita ili azifanyie kazi.

HABARI MICHEZO

# AZAM FC, SINGIDA BIG STARS SASA NI VITA NAFASI YA TATU

**Na Saada Akida**

WAKATI kila moja ikiwa imebakiza mechi nane kabla ya kuhitimisha msimu wa Ligi Kuu Bara, Azam FC na Singida Big Stars, zimeingia katika vita mpya ya kuwania kumaliza nafasi tatu baada ya kulingana kila kitu kasoro tofauti ya mabao ya kufunga na kufungwa.

**Nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara kwa sasa ni lulu kutokana na kuwapo kwa uwezekano mkubwa wa kupata tiketi ya kushiriki Kombe la Shirikisho Afrika endapo Tanzania itaendelea kutetea nafasi yake ya kuingiza timu nne kwenye michuano hiyo ya CAF.**

Katika msimamo wa ligi hiyo, Yanga ipo kileleni ikiwa na pointi 59 ikifuatiwa na Simba kwa alama zake 53, jambo ambalo linazikatisha tamaa Azam FC na Singida Big Stars kuweza kufurukuta na kuishusha miamba hiyo miwili kutokana na tofauti kubwa ya pointi kwa sasa.

Kwa sasa Azam FC ipo nafasi ya tatu ikiwa na alama 43 sawa na Singida Big Stars baada ya timu hizo kila moja kushuka kushinda mechi 13, sare nne na kupoteza michezo mitano baada ya kushuka dimbani mara 22.

Hata hivyo, Azam FC yenyewe imefunga mabao 37 huku ikiruhusu nyavu zake kutikiswa mara 23, wakati Singida Big Stars yenyewe ikicheka na nyavu mara 25 na ya kufungwa 18, hivyo 'Wanalambalamba' wana tofauti kubwa ya mabao ya kufunga na kufungwa.

Wakizungumza na gazeti hili kwa nyakati tofauti jana, makocha wa timu hizo, Kaimu Kocha Mkuu wa Azam FC, Kali Ongala na Kocha Mkuu wa Singida Big Stars, Hans Van Pluijm, kila mmoja alikiri hali kuwa ngumu ya kumaliza katika nafasi hiyo ya tatu.

Ongala alisema wana kazi ngumu mbele yao ya kuhakikisha wanashinda michezo iliyosalia kipindi hiki cha lala salama ili kufikia malengo yao.

Alisema ligi imekuwa ya ushindani na kila timu inahitaji kupata matokeo ili kujiweka salama katika msimamo huku wakihitaji kupambana kila mechi kutafuta matokeo mazuri ili kumaliza msimu huu wakiwa nafasi ya tatu.

"Tumejiondoa katika mbio za ubingwa na hata nafasi ya pili, akili na nguvu zetu tunazielekeza kutafuta matokeo mazuri katika michezo iliyosalia kutafuta pointi tatu muhimu ili tumalize msimu kwenye nafasi ya tatu katika msimamo.

"Ligi imekuwa na ushindani mkubwa kwa sababu kila timu unayokutana nayo hasa zilizopo chini ya msimamo zinahitaji kutoka zilipo na kujiweka salama mwishoni mwa msimu kufikia malengo yao," alisema Kali.

Kwa upande wa Pluijm, alisema wanafanyia kazi madhaifu yao na kujiweka imara kwa ajili ya kusaka pointi muhimu katika michezo iliyoko mbele yao kufika malengo yao ikiwamo kumaliza msimu nafasi ya tatu.

Alisema baada ya kupoteza mechi dhidi ya Simba, wamerudi uwanjani kufanyia kazi makosa yao ili kujiimarisha kwa mechi zijazo kupambana kusaka pointi muhimu.

"Tunahitaji kumaliza ligi tukiwa nafasi ya tatu, hatutaangalia waliopo juu yetu, tunafanya maandalizi mazuri kujiandaa na mchezo ijayo kufanya vizuri na kutafuta ushindi kila mechi kwa sababu ya kuhitaji nafasi ya tatu," alisema Pluijm.

Alisema anaimani na kikosi chake kufanya vizuri kwa sababu ya uwezo na ubora wa wachezaji alikuwa nao ndani ya kikosi chake kuweza kumpa matokeo chanya.

## *KVZ FC: Bado tumo mbio ubingwa Zanzibar*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya KVZ FC imesema licha ya kupoteza michezo miwili mfululizo, bado wanaendelea na nia yao ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar.

KVZ ambao walikaa kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar kwa muda mrefu, kwa sasa wametupwa nafasi ya tatu wakiwa na alama 37 baada ya kufungwa mechi mbili za mzunguko wa 18 na 19 dhidi ya KMKM na JKU.

Kwa sasa Mabaharia KMKM ndio vinara wa ligi hiyo wakiwa na alama 41 wakifuatiwa na Mlandege FC yenye pointi 38.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa KVZ FC, Ali Khalid, alisema bado wapo katika mbio za ubingwa wa ligi hiyo kwa kuwa wanaamini kwa michezo iliyobaki wanayo nafasi kubwa ya kutimiza lengo lao.

Alisema michezo miwili waliyoipoteza haijawaondoa katika malengo yao, bali imewapa nguvu na hamasa ya kufanya vizuri michezo 11 iliyosalia.

Alisema wachezaji wote bado wanahamasa na kiu ya ubingwa kwa msimu huu, hivyo hata benchi la ufundi nalo linaendelea na jitihada zake kuhakikisha wanashinda mchezo wao wa 20 dhidi ya Jamhuri FC utakaopigwa Uwanja wa Amaan Jumamosi wiki hii.



Wachezaji wa timu ya mpira wa kikapu ya vijana, wakifanya mazoezi katika viwanja vya Jakaya Kikwete Kidongo Chekundu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Ruvu yashinda baada ya mechi 13

**Na Adam Fungamwango**

HATIMAYE baada ya mechi 13 kupita, timu ya Ruvu Shooting imeonja ushindi wake wa kwanza baada ya kuhamia kwenye Uwanja wa Jamhuri Morogoro na kuichapa KMC mabao 2-1.

Ruvu iliamua kukimbilia kwenye uwanja huo badala ya Uhuru Dar es Salaam ambao ulikuwa wake wa nyumbani kutokana na kufungwa kwa uwanja wao halisi, Mabatini Mlandizi mkoani Pwani.

Msemaji wa Ruvu Shooting, Masau Bwire (pichani), alidai hawakuukimbia Uhuru kwa sababu hawafanyi vizuri, ila Jamhuri Morogoro ulikuwa ndiyo kipaumbele chao hapo awali, lakini wakaambiwa nao haukidhi vigezo ndipo waliporudi Uhuru, lakini kwa sasa wameruhusiwa kutumia Jamhuri baada ya kukidhi vigezo.

Ikiwa ni mechi yake ya kwanza kwenye uwanja huo, Ruvu iliingia na mguu mzuri kwani ilipata ushindi wake wa kwanza tangu Septemba 29, mwaka jana ilipoifunga Coastal Union mabao 2-1.



Baada ya hapo haikushinda mechi 13 mfululizo, ikiwa imepoteza jumla ya mechi tisa na sare nne, kati ya hizo tatu zikiwa ni suluhu, hivyo kuifanya kushika nafasi ya pili kutoka mkiani ikiwa na alama 17 katika mechi 22 ilizocheza hadi sasa.

Yalikuwa ni mabao ya William Patrick dakika ya 28 na Samson Joseph dakika ya 78, huku KMC ikipata bao kwa mkwaju wa penalti iliyopigwa na Nzigamasabo Steve dakika tano kabla ya mechi kumalizika.

Kocha Msaidizi wa KMC, Ahmad Ally, alisema walicheza vema na kutawala mchezo, lakini makosa madogo madogo ndiyo yaliyowafanya kupoteza mechi hiyo.

"Tumecheza vema, ukiangalia hata bao lao la pili lilikuwa ni la shambulizi la kushtukiza, hata hivyo nafasi bado tunayo kuhakikisha tunabaki Ligi Kuu kwa sababu, tuna nafasi ya kurekebisha mapungufu na sasa zinahitajika zaidi pointi kuliko kucheza vizuri," alisema kocha huyo.

Ushindi wa mechi hiyo umewafanya Ruvu Shooting kupanda nafasi moja juu hadi ya 15 ikiwa na pointi 17, ikiwa kwenye harakati za kujinasua kushuka daraja, KMC ikiwa kwenye nafasi ya 12 na pointi zake 23.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### MATIP KUPIGWA BEI LIVER

KLABU ya Liverpool itasikiliza ofa msimu huu wa majira ya joto kwa beki wao wa kati wa zamani wa Kimataifa wa Cameroon, Joel Matip, mwenye umri wa miaka 31, ambaye mkataba wake hapo Anfield unamalizika mwaka 2024. ***(Football Insider)***

### CANCELO NGUMU KUUZIKA

MKURUGENZI wa Michezo wa Bayern Munich, Hasan Salihamidzic, amesema ada ya euro milioni 70 iliyowekwa katika mkataba wa mkopo wa beki wa pembeni wa Manchester City na Ureno, Joao Cancelo mwenye miaka 28 itakuwa "ngumu" kwa klabu hiyo. ***(Mirror)***

### COUTINHO KWA MKOPO

KIUNGO wa kati wa Brazil, Philippe Coutinho, mwenye umri wa miaka 30, anahusishwa na uhamisho wa mkopo kwenda Galatasaray baada ya msimu mgumu akiwa na Aston Villa. ***(Sun)***

### MESSI MKATABA MPYA

MKURUGENZI wa michezo wa Paris St-Germain, Luis Campos, amethibitisha kuwa klabu hiyo iko kwenye mazungumzo na mshindi wa Kombe la Dunia na Argentina, Lionel Messi mwenye umri wa miaka 35, kuhusu mkataba mpya. ***(Mail)***

### CORBERAN KUINOA BROM

KOCHA Mkuu wa West Brom, Carlos Corberan, mwenye umri wa miaka 39, anawania kuchukua nafasi ya Jesse Marsch iwapo Leeds United itaamua kumtimua kocha huyo. ***(Mail)***

### MOURINHO KUREJEA CHELSEA

KOCHA wa zamani wa Chelsea, Jose Mourinho, anataka 'kurejea' Stamford Bridge kwa kipindi cha tatu na Mreno huyo mwenye umri wa miaka 60, 'alijiweka karibu' na wanunuzi wapya wakati klabu ilipoanza kuuzwa. ***(Mesport)***

### ENRIQUE ATAJWA DARAJANI

CHELSEA pia ipo tayari kumwajiri kocha wa zamani wa Hispania, Luis Enrique, mwenye umri wa miaka 52, kama kocha mpya ikiwa watamtimua, Graham Potter. ***(Fichajes)***

### AUBAMEYANG KURUDI BARCA

BARCELONA inafuatilia hali ya mshambuliaji wa Gabon, Pierre-Emerick Aubameyang katika Klabu ya Chelsea huku wakipanga kumrejesha Camp Nou mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33. ***(Football transfers)***


### GALLAGHER AFUATILIWA

KLABU ya Newcastle United itaendelea kumfuatilia kiungo wa kati wa England, Conor Gallagher, mwenye umri wa miaka 22, baada ya kufanya mazungumzo na Chelsea kuhusu uhamisho wa Januari. ***(Football Insider)***

### WILLIAMS AWANIWA LIVER

LIVERPOOL na Aston Villa zimeripotiwa kuwa tayari 'kuijaribu Athletic Bilbao katika dirisha la msimu ujao wa majira ya joto kwa kupeleka ofa kwa ajili ya winga wao wa Hispania, Nico Williams mwenye umri wa miaka 20 na kiungo wa kati wa Hispania Oihan Sancet, 22. ***(AS via Teamtalk)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MOUNT HALI TETE

**LONDON,** England

MUSTAKABALI wa Mason Mount katika Klabu ya Chelsea uko mashakani kutokana na pande hizo mbili kutofautiana kwenye mkataba mpya.

**Mazungumzo kati ya Chelsea na Mount yalisitishwa baada ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, kukataa ofa akihisi kuwa inamfanya kuwa chini ya kile ambacho wachezaji wengine waandamizi na usajili mpya wanalipwa zaidi hapo Stanford Bridge.**

●●● Hana uhakika Chelsea baada ya ujio wa Enzo Fernandez aliyesajiliwa kwa...

Mount amebakiza miezi 18 katika mkataba wake wa sasa na anataka kurudisha mshahara wake wa paundi 80,000 kwa wiki, lakini klabu hiyo inatoa kiasi kidogo kuliko inavyowalipa wachezaji ghali kama Raheem Sterling.

Mazungumzo yanatarajiwa kuanza tena katika jaribio la kuvutia chini ya utawala mpya wa Todd Boehly. Baada ya kutumia zaidi ya paundi milioni 300 kununua wachezaji Januari pekee, wachezaji kutoka akademi ya Chelsea kama Mount wanatamani kuonekana kama sehemu muhimu ya siku zijazo na si kuchukuliwa kawaida.

Mount alifuzu kupitia akademi ya Chelsea na kufanikiwa kushinda Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na klabu hiyo na kuichezea England katika michuano miwili mikubwa.

Lakini sasa hana uhakika na hadhi yake katika klabu hiyo baada ya ujio wa Enzo Fernandez aliyesajiliwa kwa ada ya pauni milioni 107.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,074,7

JACKPOT MECHI WIKI HII

TAREHE: 08,09 NA 10 FEBRUARI 2023

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 08/02/23 | 20:00 | Nurnberg vs Fortuna Dusseldorf | 2.64 | 3.34 | 2.62 |
| 02. 08/02/23 | 20:15 | Angers vs Nantes | 2.35 | 3.18 | 2.98 |
| 03. 08/02/23 | 20:15 | Toulouse vs Reims | 2.35 | 3.29 | 2.89 |
| 04. 09/02/23 | 01:30 | Bragantino SP vs Sao Paulo | 2.65 | 3.06 | 2.53 |
| 05. 09/02/23 | 02:30 | Botafogo SP vs Ituano SP | 2.52 | 2.95 | 2.74 |
| 06. 09/02/23 | 03:00 | Nacional Potosi vs El Nacional Quito | 2.21 | 3.29 | 2.91 |
| 07. 09/02/23 | 04:05 | Pumas De Tabasco vs Correcaminos Uat | 2.35 | 3.22 | 2.75 |
| 08. 09/02/23 | 11:30 | Aizawl FC vs Rajasthan United | 2.48 | 2.95 | 2.80 |
| 09. 09/02/23 | 14:00 | Gokulam Kerala FC vs Minerva FC | 2.57 | 3.01 | 2.64 |
| 10. 09/02/23 | 20:00 | Nea Salamis vs Anorthosis Famagusta | 2.63 | 3.04 | 2.77 |
| 11.10/02/23 | 00:00 | Santo Andre SP vs EC Agua Santa SP | 2.30 | 2.90 | 3.11 |
| 12.10/02/23 | 04:05 | Queretaro FC vs Club Leon | 2.60 | 3.55 | 2.45 |
| 13.10/02/23 | 11:45 | Brisbane Roar vs Central Coast Mariners | 2.81 | 3.24 | 2.43 |

KUWEKA PESA:

- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa · vodacom m-pesa · halopesa · airtel money

SEND

SportPesa

SPORTPESA.CO.TZ

PIGA *150*87#

GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# TEN HAG KUTEMA WACHEZAJI SITA



**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester, Erik Ten Hag, ana mpango wa kuwaondoa wachezaji sita klabuni hapo kwenye dirisha kubwa la usajili linalofuata katika majira ya joto.

Ten Hag katika harakati zake za kutaka kuijenga timu hiyo na kurudisha ubora wa Man United, ana mpango wa kuwaondoa wachezaji ambao anaona hawatamfaa katika mpango wake wa kuirejesha klabu hiyo katika zama zake.

Wachezaji ambao inaelezwa kocha huyo ataachana nao mwishoni mwa msimu huu ni pamoja na nahodha wa sasa, Harry Maguire, Eric Baily, Phil Jones, Alex Telles, Anthony Martial, pamoja na Aaron Wan Bissaka.

Hag ana mpango wa kukisuka kikosi chake kwa namna yake kwani anahitaji wachezaji wanaoweza kuendana na mfumo wake zaidi. Pia Man United wanahitaji kuondoa baadhi ya wachezaji ili wapate fedha za kuweza kununua nyota wengine.

Klabu hiyo inaepuka hasara ya kuongeza wachezaji kwenye timu wakati wengine wapo na hawana nafasi ndani ya kikosi.



## *Xavi akunwa na kiwango Barca*

**BARCELONA,** Hispania

XAVI amewasifu wachezaji wake wa Barcelona kwa kuendelea kuwa wavumilivu katika ushindi wao wa mabao 3-0 dhidi ya Sevilla huku viongozi hao wa LaLiga wakisonga mbele kwa pointi nane zaidi ya Real Madrid.

Barca walitawala mechi ya Jumapili pale Camp Nou kabla ya kupata bao lao kupitia kwa beki wa pembeni, Jordi Alba dakika ya 58.

Gavi aliongeza la pili dakika 12 baadaye na Raphinha, aliyesaidia bao hilo, aliongeza jina lake kwenye ukurasa wa mabao huku Barca wakifikisha ushindi wa 10 mfululizo mwaka huu.

Sevilla walilenga zaidi kulinda, wakisimamia mikwaju mitatu pekee kwa jumla ya mabao 16 ya Barca, na Xavi amefurahishwa na kikosi chake.

"Hii ilikuwa siku ya kuthubutu," aliiambia DAZN.

"Tulizungumza wakati wa mapumziko. Siku zote ni ngumu kushambulia wakati mpinzani ana wachezaji 11 nyuma ya mpira.

"Lakini tulifanya vizuri sana na nimeridhika sana na matokeo haya."

Barca walichukua fursa kamili ya mshangao wa Real Madrid kupoteza 1-0 dhidi ya Real Mallorca mapema siku hiyo na kuendeleza uongozi wao kileleni huku wakikaribia kutwaa taji la kwanza katika misimu minne.

741,067/-

# MOROCCO YAIPA MBINU TANZANIA KUTOKA KISOKA

**Na Christina Mwakangale**

ILI Tanzania iweze kupata matokeo bora na kupiga hatua kwenye michezo ikiwamo mpira wa miguu, hakuna njia ya mkato zaidi ya kufanyika uwekezaji mkubwa kuanzia kwa watoto wadogo ambao ni rahisi kuvikuza vipaji vyao kwa manufaa ya baadaye, imeelezwa.

Balozi wa Morocco nchini, Zakaria El Goumiri (pichani), ndiye alitoa kauli hiyo Dar es Salaam jana, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu masuala mbalimbali, ikiwamo michezo.

Alisema kama ilivyo nchi nyingine barani Afrika, awali Morocco ambayo ilimaliza nafasi ya nne kwenye Kombe la Dunia nchini Qatar 2022, haikufanya vizuri kwenye michezo aina mbalimbali na kwamba tangu miundombinu, vituo vya ufundishaji michezo vilipoimarika ndipo mafanikio yalipofikiwa.

**“Mpira wa miguu ndio mchezo mkubwa nchini Morocco na kwa kutoa uzoefu ni kwamba kunahitajika uwekezaji na kuwaandaa watoto, vijana kupitia vituo vya mafunzo ya michezo. Utakuwa na uhakika wa mafanikio ukiwekeza mbali na hapo utakuwa unabahatisha,” alisema Balozi Zakaria.**

“Morocco itaendelea kutoa ushirikiano kwa nchi za Afrika ambazo zinapenda kuinuka kwenye soka, kwa sababu kipaumbele chetu cha kwanza ni Afrika, sote ni kitu kimoja licha ya tofauti zetu za kijiografia,” alisema



balozi huyo.

Alisema wakati nchi hiyo inapojiandaa kuwa mwenyeji wa mashindano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (CAN), mwaka 2025, maandalizi yanaendelea vizuri ikiwamo uboreshaji wa miundombinu na hoteli.

## Yanga na jambo lao kwa Watunisia

INATOKA UKURASA 24

fara wa kikosi cha timu hiyo, lakini furaha yao ni kurejea kwa Salum Abubakari ‘Sure Boy’ na Khalid Aucho ambao wamepona na wapo fiti kwa mchezo huo.

“Baada ya mechi yetu dhidi ya Namungo FC, tumerudi uwanjani na kuendelea kufanyia kazi mapungufu yaliyojitokeza ikiwamo sehemu ya kiungo kuiimarisha kuwa bora kutokana na kurejea kikosini kwa Aucho na Sure Boy.

“Tumefanya maandalizi mazuri kwa kuwa tunatambua mchezo utakuwa wa ushindani mkubwa kutokana na sisi kuwa ugenini, tunahitaji kupata alama katika mchezo wetu huo wa kwanza katika hatua ya makundi,” alisema kocha huyo.

Tayari Yanga wametanguliza mapema maofisa wao kwenda nchini Tunisia kwa lengo la kuweka mazingira mazuri ya timu kufikia pamoja na sehemu ya kufanyia mazoezi watakapotua nchini humo.



Kocha Mkuu wa Simba, Robertinho Oliveira.

## *Sakho, Baleke fiti kuivaa Horoya*

INATOKA UKURASA 24

ezo baada ya kupata maumivu hayo hali iliyozua hofu kwa mashabiki na wapenzi wa timu hiyo, lakini nyota huyo raia wa Mali hakupata madhara makubwa.

Kwa mujibu wa Daktari wa Simba, Kagabo, Kanoute aliangukia nyonga na kupata maumivu yaliyofanya ashindwe kuendelea na mchezo, lakini halikuwa tatizo kubwa.

Wakati huo huo, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Simba, Salim Abdallah ‘Try Again’ yupo mjini Tangier nchini Morocco akishiriki kozi ya Diploma ya Uongozi wa Klabu (Diploma in Club Management) inayotolewa na Fifa.

“Hii ni fursa kubwa ambayo Simba tumepata na itatusaidia kuboresha uendeshaji wa klabu yetu, tutakuwa moja ya timu bora ambayo itakuwa mfano kwa timu zingine, wakati hili linaendelea tukumbuke pia Fifa na CAF wanaendelea na maandalizi ya Super Cup ambayo Simba tutashiriki, sisi tunaanza wengine watafuata,” alisema Try Again.

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 11/02/23 | 18:00 | Southampton FC vs Wolverhampton Wanderers | 2.75 | 3.10 | 2.60 |
| 02. 11/02/23 | 18:00 | KVC Westerlo vs KAA Gent | 2.80 | 3.30 | 2.42 |
| 03. 11/02/23 | 18:15 | UD Almeria vs Real Betis Seville | 2.80 | 3.30 | 2.44 |
| 04. 11/02/23 | 22:45 | Lazio Rome vs Atalanta BC | 2.27 | 3.35 | 3.00 |
| 05. 11/02/23 | 23:00 | Valencia CF vs Athletic Bilbao | 2.95 | 3.15 | 2.41 |
| 06. 12/02/23 | 09:00 | Macarthur FC vs Wellington Phoenix FC | 2.55 | 3.15 | 2.29 |
| 07. 12/02/23 | 15:00 | Toulouse FC vs Stade Rennes | 3.05 | 3.35 | 2.25 |
| 08. 12/02/23 | 16:00 | Getafe CF vs Rayo Vallecano | 2.75 | 2.85 | 2.80 |
| 09. 12/02/23 | 16:30 | Vitesse Arnhem vs FC Utrecht | 2.39 | 3.45 | 2.75 |
| 10. 12/02/23 | 17:00 | Angers SCO vs AJ Auxerre | 2.25 | 3.30 | 3.10 |
| 11. 12/02/23 | 17:00 | Montpellier HSC vs Stade Brest 29 | 2.35 | 3.25 | 2.95 |
| 12. 12/02/23 | 17:30 | Hertha BSC vs Borussia Monchengladbach | 2.75 | 3.50 | 2.37 |
| 13. 12/02/23 | 18:15 | RC Celta de Vigo vs Atletico Madrid | 3.40 | 3.05 | 2.24 |
| 14. 12/02/23 | 19:30 | 1. FC Cologne vs Eintracht Frankfurt | 2.65 | 3.45 | 2.47 |
| 15. 12/02/23 | 20:30 | Real Valladolid vs CA Osasuna | 2.60 | 3.05 | 2.80 |
| 16. 12/02/23 | 21:00 | Sporting Lisbon vs FC Porto | 2.75 | 3.20 | 2.55 |
| 17. 12/02/23 | 22:45 | Olympique Lyon vs RC Lens | 2.39 | 3.40 | 2.80 |


MECHI ZA USHINDI
“1” NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA “X” NI TIMU KUTOKA SARE “2” NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMANNE - 07/02/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 12:00 | 5022 | Bhayangkara Surabaya Utd vs PS Tni | 2.21 | 3.22 | 2.96 |
| 14:00 | 5688 | Mohammedan SC vs Churchill Brothers | 2.32 | 3.15 | 2.84 |
| 14:30 | 4136 | Persita Tangerang vs Persija Jakarta | 2.96 | 3.11 | 2.27 |
| 15:40 | 2858 | Hajer Club vs Al Faisaly (KSA) | 4.78 | 2.96 | 1.81 |
| 15:45 | 2374 | Smouha Club vs Al Masry Club | 3.12 | 2.68 | 2.63 |
| 16:00 | 5648 | Najran SC vs AL Hazm | 4.76 | 3.26 | 1.72 |
| 17:00 | 4719 | Kerala Blasters FC vs Chennaiyin FC | 1.90 | 3.51 | 3.46 |
| 17:45 | 3891 | AL Khalidiyah vs Al Shabbab | 1.36 | 4.24 | 7.87 |
| 17:45 | 5560 | AL Badii vs Al Hala Muharraq | 4.03 | 3.41 | 1.79 |
| 18:00 | 3484 | Talaea El Gaish vs Pyramids | 5.76 | 3.48 | 1.63 |
| 18:30 | 5696 | AL Khlood vs Al Ahli Jeddah | 4.70 | 2.85 | 1.74 |
| 20:00 | 1643 | Sandhausen vs SC Freiburg | 5.38 | 4.20 | 1.57 |
| 20:00 | 5132 | Coca Cola vs National Bank | 2.05 | 2.98 | 3.98 |
| 20:45 | 2128 | AZ Alkmaar vs Utrecht | 1.68 | 3.79 | 4.15 |
| 21:00 | 2942 | Bnei Sakhnin vs Hapoel Beer Sheva | 4.47 | 3.54 | 1.68 |
| 21:00 | 3165 | Deportivo Municipal vs Carlos Mannucci | 2.25 | 3.21 | 2.90 |
| 21:00 | 5807 | Vasas SC vs Budapest Honved | 2.15 | 3.31 | 3.00 |
| 22:00 | 2949 | De Graafschap vs De Treffers | 1.42 | 4.46 | 5.81 |
| 22:00 | 3774 | Flamengo vs Al Hilal Riyadh | 1.39 | 4.46 | 6.43 |
| 22:45 | 1151 | Maidenhead U vs Southend | 4.15 | 3.31 | 1.85 |
| 22:45 | 1282 | Grimsby vs Luton Town | 3.84 | 3.45 | 1.87 |
| 22:45 | 1457 | Eintracht Frankfurt vs SV Darmstadt | 1.56 | 4.30 | 5.38 |
| 22:45 | 1473 | Sheffield Utd vs Wrexham | 1.45 | 4.43 | 5.91 |
| 22:45 | 1592 | Salernitana vs Juventus | 5.28 | 3.77 | 1.60 |
| 22:45 | 1660 | Bath City vs Hampton and Richmond | 2.05 | 3.37 | 3.16 |
| 22:45 | 2151 | Alloa Athletic vs Falkirk FC | 3.05 | 3.42 | 2.15 |
| 22:45 | 2178 | Alfreton vs Curzon | 1.95 | 3.38 | 3.43 |
| 22:45 | 2179 | Fleetwood Town vs Sheffield Wed | 3.61 | 3.46 | 1.93 |
| 22:45 | 2314 | Halifax vs Barnet | 2.28 | 3.26 | 2.94 |
| 22:45 | 2433 | Crewe vs Leyton Orient | 3.96 | 3.26 | 1.92 |
| 22:45 | 2449 | Hungerford Town vs St.Albans | 3.53 | 3.42 | 1.91 |
| 22:45 | 2644 | Hamilton vs Queen of South | 1.75 | 3.57 | 4.03 |
| 22:45 | 2679 | Port Vale vs Accrington | 1.92 | 3.37 | 3.82 |
| 22:45 | 3327 | Spennymoor Town vs Kings Lynn | 3.01 | 3.37 | 2.13 |
| 22:45 | 3433 | Oldham vs Dagenham and Redbridge | 2.44 | 3.31 | 2.68 |
| 22:45 | 3765 | Taunton Town vs Dulwich Hamlet | 2.20 | 3.26 | 2.95 |
| 22:45 | 3830 | Utd of Manchester vs Guiseley | 1.94 | 3.73 | 3.16 |
| 22:45 | 3886 | Weymouth vs Concord Rangers | 1.70 | 3.68 | 4.15 |
| 22:45 | 4071 | Chesterfield vs Woking | 2.09 | 3.36 | 3.25 |
| 22:45 | 4123 | Burnley vs Ipswich | 1.85 | 3.44 | 3.94 |
| 22:45 | 4529 | Radcliffe Borough vs Belper Town | 1.55 | 3.99 | 4.87 |
| 22:45 | 4653 | Cheshunt vs Welling | 2.64 | 3.27 | 2.41 |
| 22:45 | 4664 | Tamworth vs Stourbridge | 1.36 | 4.57 | 6.85 |
| 22:45 | 4927 | Doncaster vs Tranmere | 2.82 | 3.17 | 2.44 |
| 22:45 | 5096 | York City vs Solihull Moors | 2.89 | 3.32 | 2.28 |
| 22:45 | 5471 | Leamington vs Buxton FC | 2.45 | 3.27 | 2.59 |
| 22:45 | 5629 | Hereford United vs Southport | 2.19 | 3.33 | 2.91 |
| 22:45 | 5740 | Poole Town vs Swindon Supermarine | 2.03 | 3.73 | 2.95 |
| 22:45 | 5999 | Blackpool vs Huddersfield | 2.17 | 3.18 | 3.28 |
| 23:00 | 5604 | NAC Breda vs Heerenveen | 4.15 | 3.63 | 1.71 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Jumanne Februari 7, 2023
Nipashe



Mount hali tete Chelsea

UKURASA 21

TUPO 'FITI'...



Jean Baleke (kushoto) na Pape Sakho, ambao walizua hofu baada ya kuumia juzi kwenye mechi dhidi ya Al Hilal Uwanja wa Benjamin Mkapa, imeelezwa watarejea leo mazoezini. Nyuma yao ni Joash Onyango wakati wakipasha katika mechi dhidi ya Singida Big Stars Ijumaa iliyopita ambayo walishinda 3-1. **MPIGAPICHA WETU**

## Yanga na jambo kwa Watunisia

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha Yanga kinaondoka leo na Shirika la Ndege la Emirates kuelekea Tunisia tayari kwa mchezo wao wa kwanza wa hatua ya makundi wa Kombe la Shirikisho Afrika utakaopigwa Jumapili wiki hii nchini humo.

Yanga itapitia Dubai na kisha kuunganisha ndege ya kwenda katika mji wa Sousse Tunisia uliopo umbali wa kilometa 140 kutoka mji watakocheza mechi hiyo dhidi ya US Monastir.

Sousse ndio mji wa nyumbani kwa Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi na ndipo ilipokuwa imeweka kambi wakati ikienda kucheza mechi ya marudiano ya mchujo kuwania kufuzu hatua ya makundi ya michuano hiyo dhidi ya Club Africain na kushinda bao 1-0.

Lakini Sousse ndio mji wa nyumbani kwa Klabu ya US Monastir watakayokutana nayo Jumapili wiki hii jijini Tunis, Tunisia.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze, alisema wana kibarua kigumu cha kuhakikisha wanashinda mchezo huo ili kupata pointi zitazowaweka katika nafasi nzuri kwenye kundi lao.

Alisema wanatarajia kumkosa nyota wao, Bernard Morrison, ambaye alimsema ni majeruhi, hivyo hatukuwapo katika msa-

INAENDELEA UKURASA 23

# Sakho, Baleke fiti kuivaa Horoya

**Saada Akida na Hadija Mngwai**

## Okrah bado shida, Robertinho atoa neno kuwavaa Waguinea hao, Fifa yamwingiza darasani Try Again...

KLABU ya Simba imewashusha pumzi mashabiki na wapenzi wa timu hiyo, kuhusu hofu ya kuwakosa nyota wawili wa kikosi cha kwanza Pape Sakho na Jean Baleke, kuelekea mchezo wao wa kwanza wa hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika baada ya juzi kushindwa kumaliza mechi dhidi ya Al Hilal ya Sudan.

**Katika mchezo huo wa kirafiki wa kimataifa uliopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam na kumalizika kwa sare ya bao 1-1 juzi, Sakho alishindwa kuendelea na mchezo baada ya kupata maumivu ya mguu wakati Baleke alitolewa uwanjani kwa machela hali iliyozua hofu kwa mashabiki wa Simba kuelekea mechi dhidi ya Horoya AC nchini Guinea Jumamosi wiki hii.**

Hata hivyo, Daktari wa Simba, Edwin Kagabo, amesema nyota hao hawakupata madhara makubwa na wanaendelea vizuri, hivyo wataanza mazoezi na wenzao leo baada ya mchezo wa juzi dhidi ya Al Hilal wachezaji wote kupewa mapumziko ya siku moja na leo kutakiwa kuanza kurejea mazoezi.

"Sakho na Baleke walipata maumivu katika mchezo wa jana (juzi), lakini hawakupata madhara makubwa, wanaendelea vizuri na kesho (leo) wataendelea na programu ya mazoezi," alisema Dk. Edwin na kuongeza:

"Kuhusu Okrah (Agustine), uwezekano wa kuanza mazoezi hivi karibuni ni mdogo kwa sababu bado anasikia maumivu ya mguu, tunasubiri vipimo vya CT Scan ili kujua ukubwa wa jeraha lake."

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa Simba, Robertinho Oliveira, ameweka wazi kuwa mechi hiyo ya kirafiki dhidi ya Al Hilal imemsaidia kupata mwanga mzuri wa kikosi chake kuelekea mchezo wa hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Horoya.

Akizungumza na gazeti hili jana, Robertinho alisema mchezo huo ameutumia kwa ajili ya kuwapa nafasi wachezaji ambao hawakupata kuonekana katika michezo iliyopita ili kujiandaa kwa mechi kubwa zijazo.

Alisema kama benchi la ufundi imewasaidia kuona madhaifu na ubora wao kabla ya kwenda nchini Guinea kuanza kampeni yao ya kutafuta pointi muhimu katika michuano hiyo ya Ligi ya Mabingwa.

"Mechi ilikuwa nzuri na kipimo kizuri kwetu kuna wachezaji nimewaona ambao hawajacheza mara kwa mara katika ligi, tupo kwenye maandalizi ya mchezo wetu wa kimataifa dhidi ya Horoya AC, tunahitaji kupata matokeo mazuri.

"Nimeona madhaifu na ubora wetu baada ya kuona vijana wangu hao na baadaye kuwapa nafasi wachezaji wa kikosi cha kwanza ili kuona kile ambacho nimekielekeza mazoezini kinafanyiwa kazi," alisema Robertinho.

Alisema alifurahi kuona nyota wake wa kikosi cha kwanza wakiingia na kubadilisha mchezo hadi kusawazisha bao katika mchezo huo wa kirafiki, hivyo anatarajia makubwa kutoka kwao katika mchezo ujao.

Katika hatua nyingine kiungo Sadio Kanoute naye atarejea uwanjani baada ya kupewa mapumziko ya siku mbili baada ya kuumia katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Singida Big Stars, uliopigwa Ijumaa iliyopita.

Kanoute alitolewa dakika ya 83 ya mch-

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >